# Nipashe

Jumanne Desemba 29, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580444

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



TESA

KERO ZILIZOUDHI WENGI

TEKNOLOJIA

DOZI YA KUFANIKIWA NA 'KUPAA' KIMAISHA 2021

UKURASA 20

**Maziko** ya miili 4 familia moja yaibua mazito

UKURASA 5



**Mwinyi** aunda tume uchunguzi kuporomoka jengo la ajabu

UKURASA 17

# Waziri aingilia kati kilio bando, vifurushi

UKURASA 2



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile (wa pili kushoto) na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Mhandisi Kundo Mathew (wa tatu kushoto), wakimsikiliza Mhandisi Jumanne Ikuja, akiwaelezea kuhusu gari lenye mitambo maalumu linalofuatilia matumizi ya masafa wakati wa ziara yao, katika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Dar es Salaam. Wanne kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Mhandisi James Kilaba. **MPIGAPICHA WETU**

## JPM amtumbua Mkurugenzi akiwa safarini

UKURASA 4



## Abiria mikoani wahangaika kurudi Dar

UKURASA 2

**MICHEZO** **SVEN ACHEFUKA SIMBA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Katibu wa Chama cha Wachimbaji Madini (MAREMA) Tawi la Mirerani, Rachel Njau, akisoma tamko la kulaani taarifa potofu iliyosambazwa mitandaoni kwa kumhusisha Waziri wa Madini, Dotto Biteko, kuwahujumu wachimbaji. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro, Awadhi Omary na Mwenyekiti wa MAREMA, Peter Laizer, juzi. PICHA: GIFT THADEY **PICHA: SABATO KASIKA**

# Abiria mikoani sasa wahangaika kurudi Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WINGI wa abiria wanaosafiri kwenda kusherehekea sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwenye maeneo mbalimbali nchini, umesababisha uhaba wa mabasi na baadhi yao kujikuta wakikesha kwenye vituo kwa kukwama kupata usafiri.

Kila mwaka mwezi Desemba abiria husafiri kwa wingi kwenda sehemu mbalimbali kusherehekea sikukuu hizo na kuwa chanzo cha kuwapo kwa uhaba wa usafiri.

Nipashe ilitembelea katika stendi kuu za mabasi ya mikoani katika Mkoa wa Arusha, Mwanza, Mbeya, Kilimanjaro na kukuta idadi kubwa ya abiria waliokwama wakisubiria magari kwa ajili ya safari, huku baadhi yao waliobahatika kusafiri wakieleza ugumu walioupata kupata tiketi.

**ARUSHA**

Tofauti na uhaba wa usafiri pia mji wa Arusha, umekuwa na ongezeko la watu na wakati mwingine kumesababisha foleni katika baadhi ya maeneo ya ndani na nje ya mji huo.

Vicent Kimario, msafiri kutoka Arusha, kwenda Moshi, mkoani Kilimanjaro aliiambia Nipashe kwamba tangu Desemba 23, kulikuwa na shida ya kupata usafiri.

David Patrick, ni msafiri kutoka Arusha, kwenda Mkoa wa Singida, alisema alifika stendi majira ya saa 6:00 asubuhi, lakini hadi mchana gari halikufika kituoni hapo, ilhali alishakata tiketi mapema.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Laila Hassan, aliiambia Nipashe kuwa kipindi cha sikukuu maofisa wa LATRA hufanya ukaguzi kuhakikisha abiria wanasafiri salama.

Alisema kutokana na udhibiti wa mamlaka hiyo, wamefanikiwa kupunguza tatizo la abiria kupandishiwa nauli.

Alisema kwa maeneo yenye tatizo la usafiri mamlaka hiyo, inatoa vibali vya usafiri kwa magari yenye sifa ili kutatua tatizo hilo.

**MBEYA**

Katika kituo kikuu cha mabasi mkoani Mbeya, baadhi ya wasafiri walisema kuna ugumu wa kupata usafiri.

Walisema hali hiyo imetokana na mabasi yanayosafirisha abiria kutoka mkoani humo kwenda mikoa mingine kutokuwa na nafasi kwa zaidi ya siku mbili.

Mwenyekiti wa Stendi Kuu ya Mkoa wa Mbeya, Salum Kilowoko, alisema idadi ya mabasi yanayosafirisha abiria inaridhisha kwa vile magari ni mengi, lakini kutokana na wingi wa abiria magari yanakuwa yameshakatisha tiketi na kujaa kwa zaidi ya siku mbili au tatu kabla ya safari.

Kilowoko alisema kwa kawaida nauli za kutoka Mbeya hadi Mwanza kama zilivyoainishwa na LATRA Sh. 55,000, lakini wakati ambao hakuna msongamano wa abiria watu hupunguziwa hadi Sh. 45,000 kitu ambacho hakiwezekani.

**KILIMANJARO**

Baadhi ya abiria wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza magari ya mikoani.

"Ifike mahali serikali na mamlaka zilizopo zihakikishe zinaratibu usafiri kwa mabasi ya mikoani, ili usumbufu unaojitokeza nyakati za sikukuu usijirudie," alisema Monica Massawe.

**MWANZA**

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Mwanza, Halima Lutazi, alisema wamejipanga dhidi ya magari yanayokatisha safari, pamoja na yale yanayofanya udanganyifu kwenye nauli.

Lutazi alisema hali ya usafiri iko salama licha ya magari kuiba ruti na kupandisha nauli ambayo aliikemea.

Lutazi alisema tayari wamewakamata baadhi ya watu wenye magari na kuwalipisha faini na msako unaendelea kila siku kuanzia asubuhi hadi jioni, ili kuwabaini wenye magari wanaofanya mchezo huo.

Alisema wenye magari wanalazimisha kutoa huduma katika maeneo ambayo hawakupangiwa na kuacha kule walipopangiwa na kwamba watu wa aina hiyo wataendelea kusakwa.

Ofisa huyo wa LATRA alisema kutokana na watu wengi kutaka kusafiri katika kipindi cha likizo ya mwisho wa mwaka, wanalazimika kushinda stendi ya mabasi ya Nyegezi kusimamia utekelezaji wa sheria.

Nipashe lilizungumza na baadhi ya abiria waliokuwa kituoni ambao walilalamikia kuzidishiwa nauli tofauti na ilivyokuwa siku za nyuma.

Nyamizi Abdala ni miongoni mwa abiria waliokumbwa na kadhia hiyo, alisema mbinu wanazotumia wenye mabasi wanamlazimisha abiria kulipa bei kubwa, lakini tiketi wanaandika bei ya chini.

***Imeandaliwa na Nebart Msokwa (Mbeya), Allan Isack (Arusha) Mary Mosha (Moshi) na Richard Makore (Mwanza)***

# Waziri aingilia kati kilio bando, vifurushi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, ameipa miezi mitatu, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kumaliza malalamiko ya 'bando' na vifurushi yanayotolewa na wateja dhidi ya kampuni za simu.

Waziri Ndugulile aliyasema hayo jijijini Dar es Salaam, wakati alipoitembelea TCRA ikiwa ni moja ya taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kwa lengo la kufahamiana, kutambua majukumu yao na kuzungumza na bodi, menejimenti na wafanyakazi wake.

Pia, lengo la ziara hilo ni kuwa na uelewa wa pamoja na kushirikiana kufanya kazi ya kuhudumia wananchi kuelekea mapinduzi ya viwanda, kuiwezesha Tanzania kuwa na uchumi wa kidijitali.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano serikalini Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ilisema, waziri aliitaka TCRA ishughulikie malalamiko ya wananchi kwa kuwa hawana imani na vifurushi na 'bando'.

Pia, aliitaka kuhakikisha kunakuwapo na mfumo wa kuhakiki gharama halisi za mawasiliano kuendana na fedha aliyotoa mteja na kuwe na namba ya bure ambayo wananchi watapiga ili kuwasilisha malalamiko yao waweze kuwa na imani na serikali yao.

Ndungulile aliitaka TCRA kushirikiana na Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA - CCC), kumaliza tatizo hilo kwa maelezo kuwa Watanzania si wajinga.

Aliwaambia kuwa mteja anataka aone kapata Sh. moja na anaitumia fedha yake hiyo kupiga simu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, alihimiza wahakikishe kuwa 'chaneli' tano za bure za runinga zinaonekana hata baada ya muda wa kulipia kumalizika kwa kuwa hazionekani kwenye baadhi ya ving'amuzi.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Kundo Mathew, aliipongeza TCRA kwa kutengeneza mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kutambua matatizo yaliyopo na imejipanga kuyafanyia kazi kwa kuwa lazima ichukue nafasi yake na iwafikishe Watanzania wanakotaka kwenda.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Zainab Chaula, aliwataka wafanyakazi wa TCRA kujiongeza na kujituma zaidi badala ya kusubiri maagizo na maelekezo.

Aliwataka wafanye hivyo kwa kuwa ni wataalamu na kwamba washirikiane kwa pamoja, ili waendelee kuwahudumia watoa huduma na watumiaji wa bidhaa za mawasiliano.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, alikiri uwapo wa tatizo la bando na vifurushi na kuahidi kulifanyia kazi kwa kuwa TEHAMA imeongeza mnyororo wa thamani kwenye sekta zote na imesogeza huduma mbalimbali viganjani kwa wateja.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yaunda kamati kuchunguza moto Kagera

**Na Restuta Damian,**

KARAGWE

SERIKALI imeunda kamati maalum kuchunguza chanzo cha moto uliotokea juzi na kuteketeza maduka matano, saluni na mgahawa katika Kata ya Kayanga, wilayani Karagwe, mkoani Kagera.

Kamanda wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji mkoani Kagera, Hamisi Dawa, alisema tume hiyo inashirikisha kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ya Karagwe ambayo itakuwa na kazi ya kufanya uchunguzi wa kina ili iweze kuja na majibu.

Ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia juzi na moto huo ulianzia kwenye duka moja na kusambaa kwenye maduka mengine.

"Tukio hilo lilitokea pale Kayanga mjini duka moja lilianza kushika moto na mengine halafu yakafuata mengine na maaskari wetu walifika eneo la tukio na kuanza kupambana kuzuia moto," alisema Dawa.

Aidha, Dawa alisema moto huo uliteketeza maduka matano na stoo zake, saluni moja na mgahawa ambao hasara na gharama za mali zilizokuwamo haijajulikana bado.



Kiongozi na Sheikh Mkuu wa Waislamu Shia Ithnasheriya Tanzania Maulana, Hemed Jalala, akitoa salamu za Krismasi na Mwaka Mpya kwenye Masjid Ghadir Kigogo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Sheikh Said Athumani Imam wa Masjid Ghadir, tawi la Jumuiya ya Waislamu Shia Ithnasheriya Tanzania (TIC). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM akagua ujenzi daraja

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana, amekagua maendeleo ya ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi ambalo litakuwa na urefu wa kilometa 3.2 na kuwa daraja refu Afrika Mashariki na Kati.

Daraja hilo ambalo linajengwa na mkandarasi China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa gharama ya takribani Sh. bilioni 700, linatarajiwa kukamilika Februari 2024.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara mkoani Mwanza (TANROAD), Mhandisi Vedastus Maribe, alisema ujenzi wa daraja hilo ulioanza Februari 25, 2020 umefikia asilimia 11.18 ikiwamo ujenzi wa daraja la muda ambao umefikia asilimia 51.6 na kwamba hadi kukamilika kwake linatarajiwa kuwa na nguzo 67 zikiwamo tatu kubwa.

Akizungumza baada ya kujionea kazi ya uchimbaji wa mashimo yenye urefu wa mita tatu ndani ya mwamba kwa ajili ya ujenzi wa nguzo hizo, Rais Magufuli ameelezea kufurahishwa na hatua iliyofikiwa, lakini amemtaka mkandarasi CCECC kuongeza kasi ya ujenzi kwa kufanya kazi usiku na mchana ili likamilike haraka na kuanza kutumika.

Rais Magufuli alisema daraja hilo lina umuhimu mkubwa kwa Watanzania na nchi jirani za Uganda, Burundi, Rwanda na DRC, pia amesimulia mkasa uliosababisha aweke dhamira ya kuhakikisha linajengwa na yeye ni mmoja wa walionusurika kufa maji baada ya mtumbwi aliokataa kuupanda kuzama na kusababisha vifo vya watu 11 waliokubali kupanda mtumbwi huo, ili kuvuka kutoka Busisi kwenda Kigongo.

Aliwapongeza wananchi wa Kanda ya Ziwa kwa kujengwa kwa daraja hilo ambalo litaepusha ajali za mara kwa mara za kuzama kwa mitumbwi inayovusha watu na bidhaa mbalimbali kati ya Kigongo na Busisi.

Alitoa wito kwa wananchi hasa vijana wanaopata ajira katika mradi huo, kufanya kazi kwa bidii na uadilifu badala ya kuiba vifaa vya ujenzi.

Halikadhalika, Rais Magufuli aliwapongeza Watanzania wote kwa kuchapakazi na kulipa kodi ambayo ndio inatumika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa daraja hilo na kutoa wito kwa kila Mtanzania kuhakikisha analipa kodi ipasavyo na kudai risiti kila anapofanya ununuzi wa bidhaa.


UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF WATER
ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY (EWURA)

## Employment Opportunities

**The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) is an independent, world class regulatory authority responsible for licensing, tariff and quality of service regulation of electricity, water, petroleum and Natural gas sectors. EWURA has the following vacancies for which suitably qualified Tanzanians are invited to apply.**

**1. CORPORATE AFFAIRS DIVISION**

a) Post Title : Finance Manager
b) Duty Station : EWURA Head Office -Dodoma
c) Reports to : Director of Corporate Affairs

Finance Manager will be responsible for ensuring timely and effective provision of financial services to the Authority.

d) Duties and Responsibilities:

(i) To provide support in ensuring timely and effective provision of financial services to the Authority;
(ii) To monitor collection of all revenues of the Authority on timely basis;
(iii) To provide support in monitoring financial expenditure as per Approved budget, procedures and policies;
(iv) To provide support in overseeing establishment and application of systems and procedures for finance;
(v) To provide support in ensuring that all approved and normal operations pertaining to finance are carried out on time and according to approved budget;
(vi) To provide support in overseeing prudent management of Authority's resources, including keeping records on their utilization;
(vii) To prepare time-based reports on financial performance;
(viii) To prepare operating and capital expenditure budget;
(ix) To prepare annual financial statements and provide required support to external auditors;
(x) To control, apply and monitor routine finance functions;
(xi) To monitor and control all debtors and creditors and;
(xii) To undertake any other duties as assigned by the supervisor.

e) Academic Qualifications and Experience

The ideal candidate for this position should have the following qualifications and experience:
(i) University Degree/ Advanced diploma majoring in accounting or finance from a recognized higher learning institution;
(ii) Master's Degree majoring in accounting or finance or business administration;
(iii) Possession of Certified Public Accountant, CPA(T) or ACCA Certificate;
(iv) Must be registered with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) in the category of either Associate Certified Public Accountants (ACPAs) or Associate Certified Public Accountant in Public Practice (ACPA-PPs) or Fellow Certified Public Accountants (FCPAs);
(v) Knowledge and Competence in Information and Communications Technology (ICT) application, and familiarity with one of the accounting software;
(vi) A strong knowledge of International Financial Reporting Standards (IFRS) and International Public Sector Accounting Standards (IPSAS);
(vii) Not less than seven (7) years' work experience in relevant fields out of which three (3) years should be in senior position;

a) Post Title : Human Resources Officer
b) Duty Station : EWURA Head Office - Dodoma
c) Reports to : Senior Human Resources Officer

Human Resources Officer will be responsible for assisting implementation of human resources policies, systems and procedures of the Authority.

d) Duties and Responsibilities:

(i) To participate in implementation of Open Performance Review and Appraisal System;
(ii) To participate in overseeing proper attendance to staff welfare issues;
(iii) To participate in coordination of training, learning and staff development programs;
(iv) To participate in the recruitment process;
(v) To participate in the preparations of payroll.
(vi) To maintain staff records and database.
(vii) To undertake any other duties as assigned by the supervisor.

e) Academic Qualifications and Experience

The ideal candidate for this position should have the following qualifications and experience:
(i) Bachelor's degree in human resources management or public administration;
(ii) Possession of knowledge and applications of Tanzania Labour Laws is an added advantage;
(iii) Knowledge and Competence in Information and Communications Technology (ICT) application; and
(iv) No prior work experience is required.

a) Personal Attributes

In addition to the above skills and qualifications, applicants for the above positions are required to have the following attributes:
(i) A very high level of integrity, honesty and sense of responsibility;
(ii) Ability to work under pressure and produce expected results;
(iii) Ability to work in a dynamic team;
(iv) Ability to self-manage, achieve results and meet deadlines; and willingness to work beyond the call of duty.

b) Tenure and Remuneration

(i) A competitive salary will be offered to the right candidates for the posts.
(ii) EWURA is an equal opportunity employer.
(iii) Staff will be employed on permanent and pensionable terms.

c) Mode of Application

Application letter with Curriculum Vitae (CV) including e-mail address or daytime contact telephone number, together with photocopies of certificates, one passport size photo and names and contacts of three referees should be addressed to reach the under-mentioned by 8th January, 2021.

Only short- listed candidate meeting the above criteria will be invited for interview. Lobbying and canvassing for employment will not be entertained and may work to the candidate's disadvantage.

Application letter should be addressed to:

**The Director General,**
**Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA), EWURA House, Plot No 3, Block AD, Medeli West,**
**P O Box 2857, DODOMA**

# Rais Magufuli amtumbua mkurugenzi akiwa safarini

**Na Christina Mwakangale**

RAIS John Magufuli ametengua uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, Revocatus Kuuli, kutokana na tuhuma zinazomkabili ikiwamo kujitwalia ardhi ya wananchi bila kufuata utaratibu.

Pia tuhuma nyingine ni utendaji kazi usioridhisha na ubadhirifu wa fedha za maduhuli ya serikali.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, Rais Magufuli alitangaza uamuzi huo jana wilayani Igunga, mkoani Tabora, wakati akiwasalimu wananchi wa eneo hilo akiwa safarini.

Alisema pia Rais alipata fursa ya kuwasalimu viongozi wa Tabora na kueleza kero zao.

Kadhalika, Rais Magufuli alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Phillemon Sengati, kuteua mtumishi mwadilifu atakayekaimu nafasi ya mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga hadi uteuzi mwingine utakapofanywa.

Pia, rais alisema pamoja na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, ana taarifa nyingi kuhusu dosari za Kuuli, na kwamba alishamwonya kwa vitendo vyake hivyo vya kuwadhulumu wananchi, wakiwamo wanawake.

Rais Magufuli alisema serikali anayoiongoza haiwezi kumvumilia kiongozi wa namna hiyo.

Pia taarifa, hiyo ilisema, Rais Magufuli amewashukuru wananchi wa Igunga na Watanzania kwa ujumla kwa kumchagua kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili na kuahidi kuwatumikia kwa uwezo wake wote.

Pia, aliwapongeza wananchi wa Mkoa wa Tabora, pamoja na Wilaya ya Igunga na Nzega kwa kupata maji kutoka Ziwa Victoria na kuwasihi kuyatumia vizuri kwa manufaa yao.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Yapi Markez, inayojenga reli ya umeme, wakiendelea na kazi Buguruni jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Bashungwa aahidi kurejesha heshima ya michezo nchini

**Na Shamimu Nyaki**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, amesema kuwa katika uongozi wake atahakikisha heshima ya michezo inarejea.

Bashungwa aliyasema hayo jana, jijini Dar es Salaam, katika kikao na makocha pamoja na wanamichezo wa zamani na kueleza kuwa serikali imeanza kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo.

"Lengo la kikao hiki ni kupokea mawazo kutoka kwenu namna bora ya kuendesha michezo, ili tupate mafanikio kama ambayo tulipata hapo zamani wakati nyie mkilitumikia taifa letu katika soka," alisema.

Pia alisema marekebisho yaliyofanywa katika Sheria za Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ya mwaka 1967 kuhusu michezo ya ridhaa na kulipwa, kwa hivi sasa inatambua michezo ya

kulipwa na kuna wachezaji zaidi ya 2,000 wanaocheza michezo ya kulipwa ndani ya nchi na wanamichezo takriban 28 wanacheza michezo ya kulipwa nje ya nchi.

Aliwapongeza wachezaji wa zamani kwa jinsi walivyojituma kwa nidhamu na moyo wa kizalendo kuipigania nchi na kufanikiwa kufuzu katika mashindano ya AFCON mwaka 1979.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Abdallah Ulega, ameiagiza Idara ya Michezo kusimamia maazimio yote ya kikao hicho kufanyiwa kazi.

# Ongezeko la watu tishio Hifadhi ya Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu,**

NGORONGORO

MAMLAKA ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro (NCAA), imesema kuwa matumizi ya eneo hilo kwa binadamu na uhifadhi yamefikia pagumu kunakohitaji hatua za haraka ili kuiokoa.

Akizungumza jana na kujibu maswali ya waandishi wa habari katika semina ya wahariri na waandishi waandamizi wa uhifadhi, Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Freddy Manongi, alisema kamisheni ya kuchunguza na kuja na matokeo ya kisayansi juu ya namna ya kulitumia eneo hilo kwa pamoja imefanya kazi yake.

Alisema kwa sasa hali ni ngumu kwa uhifadhi kwa kuwa kila hatua inayochukuliwa kwa ajili ya uhifadhi ina athari kwa wananchi wanaoishi ndani ya eneo hilo, na kila shughuli za kibinadamu zinazofanyika zina athari kwa uhifadhi, na kwamba idadi ya watu imeongezeka kutoka 8,000 mwaka 1959 hadi 100,000 kwa sasa.

"Najaribu kuitazama Ngorongoro miaka 10 ijayo kwamba itakuwa katika hali gani kama kasi ya watu itakuwa hii, shughuli za uhifadhi zitakuwa ngumu, migogoro baina ya jamii na wanyama itaongezeka, tutawezaje kwenda pamoja na maendeleo endelevu ya binadamu na uhifadhi," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Manongi kila kinachofanyika kwa ajili ya uhifadhi imekuwa na athari kwa binadamu, na kila kinachofanywa na binadamu kina athari kubwa kwa jamii, malalamiko mengi kwa jamii.

Mathalani, alisema hivi karibuni alipigiwa simu na diwani mmoja wa kata mojawapo ndani ya Ngorongoro ambaye alimjulisha kuwa fisi wameua kondoo 30 na kuomba hatua zichukuliwe, kulishughulikia suala hili ni kazi ngumu sana na ni ngumu kulinda kila kaya ndani ya eneo," alibainisha.

Kuhusu kamisheni iliyoundwa mwaka 2019, ilihoji watu mbalimbali na ilimaliza kazi Mei mwaka jana, na mapendekezo ya awali ilikuwa ni kuligawa eneo la Ngorongoro kwa kanda kulingana na shughuli zilizopo.

Awali, Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, alisema wizara inatambua na kuthamini mchango wa wanahabari katika kuhabarisha, kuelimisha na kuhamsisha jamii katika masuala mbalimbali ya sekta ya maliasili na utalii, mchango ambao umesaidia kufikisha taarifa kwa wingi.

"Watalii wanapopanga safari zao kuja Tanzania au kungine duniani wana taswira kuhusiana na anakokwenda kabla ya kupanga safari zao, na inatoka shuleni walikosoma au habari wanazosoma, kuona na kusikia kwenye vyombo vya habari," alisema.

Dk. Nzuki alisema; "Taswira nzuri kabla ya safari, wakati wa safari na baada ya safari ambayo itawezesha kuendelea kutangaza utalii nchini ni muhimu sana. Tuwajengee taswira kutokana na habari wanazosikia, kwenye televisheni, redio, mitandao na magazeti, tuna kazi kubwa ya kujenga taswira chanya itakayosambaa duniani kote."

Mathalani, alisema hali ya Covid-19 nchini itajionyesha zaidi kupitia vyombo vya habari kwa jinsi watu walivyokaa kwenye mkutano kwa kusogeleana na hakuna aliyevaa barakoa, jambo linalodhihirisha kuwa Tanzania ni salama na kila mmoja anaweza kuja na kurudi salama.

"Ujenzi wa taswira utasaidia, tukwepe kujenga taswira hasi kwa kuwa uzalendo ndiyo muhimu sana katika kazi ya uandishi wa habari, ili kujenga taswira chanya kusaidia kutangaza utalii duniani na kuonyesha jinsi nchi ni salama," alisema.

Eneo la Ngorongoro lilianza mwaka 1959 baada ya kumegwa kutoka Serengeti Game Reserve na kuunda Hifadhi ya Taifa ya Serengeti iliyopo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), kwa watu 4,000 kuhamishiwa ndani ya eneo na kuwa na jumla ya watu 8,000 ambao wameongezeka na sasa ni zaidi ya 100,000.

HABARI KITAIFA

# Maziko miili 4 familia moja yaibua mazito



Majeneza ya miili ya watu wanne wa familia moja waliofariki dunia kwa ajali ya moto, Sahare mkoani Tanga. **PICHA: IDDA MUSHI**

**Na Idda Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameongoza mamia ya waombolezaji kwa ajili ya shughuli ya maziko ya watu wanne wa familia moja waliofariki dunia kwa ajali ya moto huko Sahare, mkoani Tanga.

Maziko hayo ya Sigifrid Sisti Kimbi, mkewe Aurelia Kimbi na watoto wao Samuel na Ezra, yamefanyika kitongoji cha Kisomboko, Kijiji cha Kitandu, Kata ya Uru Kusini katika Wilaya ya Moshi.

Dk. Mghwira alieleza serikali kupokea kwa majonzi msiba huo, ambao umeonyesha pia upendo kwa familia iliyopoteza maisha kutokana na namna walivyokutwa wamejikunyata wakijaribu kuokoana bila mafanikio.

Aliwataka wananchi hususani wa Mkoa wa Kilimanjaro kuzingatia ujenzi unaoweka dirisha la dharura kwenye kila chumba na kuwaelekeza watoto namna ya kujiokoa ajali ya moto ikitokea, badala ya kufunga milango ya chuma isiyo na namna yoyote ya kujiokoa wakati wa dharura.

"Na nyie vijana msio na kazi muache tamaa na wizi, kwenye hivyo vidirisha tutaweka shoti ya umeme, ili ukijaribu kuingia unaswe ufe, inasikitisha kuona vijana hawana kazi wanategemea wizi na wengine ni walevi hadi wameharibu jina hasa huko maeneo kama Rombo, ambako wanaume wanalewa hadi wanajigalagaza barabarani," alisema Mghwira.

Kadhalika alieleza kusikitishwa na kitendo kilichojitokeza katika maziko ya wanafamilia hao baada ya viongozi wake wa kanisa kukataa kumzika marehemu kwa ibada ya misa takatifu kwa madai kuwa mume na mke hawakuwa na ndoa ya kanisani na akasema ni vyema viongozi wa dini wakaache kuhujumu marehemu.

"Kama mnaona waumini wenu wanakwenda kinyume, nyie ndio wa kuwasogeza karibu na kuwasahihisha, badala ya kusubiri kumhukumu marehemu, nazungumza hili kwa viongozi wote wa dini, muache kuwasimanga marehemu, wazikeni kwa heshima kwa kutangaza mazuri yao," alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Alisema ingekuwa ibada haijaanza, angeendesha yeye kwa imani yake, kwa kuwa marehemu alichopaswa kufanyiwa ni kuzikwa kwa heshima kwavile hata jamii aliyokuwa akiishi nayo ilimjengea heshima kubwa na waliishi na familia yake kwa upendo.

"Basi kama imani hamtaki kumzika zikeni hata kimila, kiserikali watu waliishi zaidi ya miezi sita ni wanandoa kamili, sasa hawa wanazaidi ya miaka minane pamoja, na wakati mwingine milolongo mirefu ya mahitaji ndio imekuwa ikichangia wachelewe kufunga ndoa, hii ni mara kadhaa sasa nasikia marehemu wakisimangwa, na sio Katoliki peke yao hata Lutherani, Anglikana, Waislamu na madhehebu mengine, nasema acheni kabisa," alisisitiza.

Awali, Paroko wa Parokia ya Kanisa Katoliki la Maonano Mawela, Padre Crispin Jumanne, alisema amefika eneo hilo kutoa pole, na alikuwa na maziko mengine kwa watu wengine watatu waliofariki katika Parokia hiyo na kusema kutokana na vikwazo vya kiimani walivyokuwa navyo marehemu hao, wasingefanyiwa ibada takatifu.

"Mmekaa kimya hapa, lakini tukiendesha ibada mtaanzia kutangaza mambo ya kibaguzi, siwasimangi marehemu, lakini nasema wengine mjifunze namna ya kuishi kwa kufuata imani zenu wakati mkiwa hai," alisema Paroko huyo ambaye alishiriki kuombea miili na kuisindikiza kaburini kwa baraka.

Mama na watoto wake wawili walifariki usiku wa kuamkia Desemba 26 baada ya nyumba yao kuteketea kwa moto huko eneo la Kwa Baba Ubaya Sahare, jijini Tanga na baba wa familia alifariki siku moja baadaye alipofikishwa Hospitali ya KCMC akitokea Bombo alikolazwa awali baada ya kujeruhiwa.




**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# Tusifute kesi hizi ni hatari

**TAARIFA** za kesi za kunajisi mtoto kuondelewa mahakamani kwa ukaidi wa mashahidi zilizochapishwa na gazeti letu leo, zinatulazimisha kuomba serikali na wadau kuwa na jitahada mpya kukabiliana na uhalifu huu.

Inaelezwa kuwa Mahakama ya Mkoa wa Wete imefutilia mbali shtaka la mtoto wa miaka 16 kumnajisi mwenzake mwenye miaka mitano, baada ya mashahidi kukataa kufika mahakamani.

Taarifa zinaeleza kuwa aliyenajisiwa ni mtoto mdogo wa kiume na kwamba shauri hilo lipo muda mrefu mahakamani bila ya kusikilizwa kwa vile mashahidi hawaonekani.

Si nia yetu kurejea kilichotokea mahakamani, lakini tunashauri serikali na wadau wa haki za watoto na sheria kutizama upya Sheria ya Makosa ya Kujamiiana na ile ya Watoto ya mwaka 2009, Kanuni ya Adhabu na mwenendo mzima wa kesi hizo.

Suala la kukaidi kufika mahakamani hasa kwenye mashauri ya kunyanyasa watoto kijinsia na kingono , ubakaji wa wanawake na mimba kwa watoto na wanafunzi limekuwa likipigwa mpira na mara nyingi mashtaka kufutwa.

Kuna maelezo kuwa wazazi, walezi , watuhumiwa na jamaa zao wanalindana ili kupoteza ushahidi na kuzima kesi hizo.

Sote tunasikia kuwa walalamikaji wanalipwa na suala linamalizwa nje ya mahakama. Mathalani, binti akipata ujauzito analalamika polisi na kuonyesha ushirikiano, lakini inapotokea aliyembaka anaahidi kuwalipa wazazi au walezi na kumtunza, anakana kila kitu kizimbani.

Inakuwa ni njia rahisi ya kukwepa mkono wa sheria kwa wanaobaka watoto, wanaonajisi na wanaofanya kila aina ya uhalifu dhidi yao kwa vile hakuna ushahidi. Inarahisisha kazi kwa mwendesha mashtaka ambaye anafuta kesi.

Tunaomba serikali ya Zanzibar pamoja na ya Muungano zitazame upya mazoea haya ya kuikwepa sheria kwa sababu yoyote inawaumiza watoto, wanawake na wanyonge na kuongeza uhalifu kwenye jamii.

Mapitio ya sheria yafanyike ili kuwakamata na kuwahukumu wazazi, walezi na jamaa wengine ambao ndugu zao watahusika kwenye kulinda wahalifu wanaonajisi au kudhulumu watoto kingono.

Sheria pamoja na kuharamisha matendo hayo pia itamke wazi jinsi ya kukabiliana na kesi hizo hasa pale mashahidi wanapokataa kufika mahakamani au walalamikaji wanapokataa kushirikiana na mahakama.

Licha ya kwamba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeingia kwenye kesi hizo za mimba utotoni na hata nyingine zinazohusiana na masuala ya kujamiiana, ni vyema pia sheria ya TAKUKURU ikarekebishwa ili ihusike moja kwa moja kuwabana wazazi, walezi na jamaa wanaoshirikiana kuzuia ushahidi mahakamani.

Tukumbuke wahalifu wakiachwa kunajisi, kuwapa ujauzito na hata kuwaambukiza maradhi watoto bila mienendo hiyo kukomeshwa ni hatari kwa taifa letu ambalo pamoja na kuwa na raia wahalifu tutakuwa pia limelea na kupalilia mienendo ya mmomonyoko wa maadili.

Tunaziomba serikali zichukue hatua kwa sababu kesi nyingi za makosa ya kujamiiana hazisikilizwi katika mahakama zetu kwa sababu ya kukosekana ushahidi na sasa ni mazoea.

Ni wazi kuwa haya ni mambo yanayotokea kote Bara na Visiwani na huenda vijijini mambo yakawa magumu zaidi kwa vile hata kiwango cha uhamasishaji ni kidogo.

Tunasikitika kuwa washtakiwa hawaadhibiwi, huku matendo hayo yakiongezeka kwenye jamii, mahakama zinapuuzwa hata zinapowapa hati ya kuitwa shaurini kama mashahidi hawatokea tena bila kuwa na sababu za msingi. Ndiyo maana tunaomba serikali zichukue hatua kunusuru taifa letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ujenzi madarasa uwe mkakati wa kudumu

**WANAFUNZI** 759,706 wamechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwaka 2021, lakini miongoni mwao watalazimika kusubiri ujenzi wa madarasa mapya ili waanze masomo.

74,166 watakaolazimika kusubiri hadi ujenzi wa madarasa ukamilike ikiwa ni sawa na asilimia 8.9 ya waliochaguliwa. Watoto hao watabaki nyumbani kwa kuwa hawakupangiwa shule katika awamu ya kwanza.

Kutokana na uhaba wa madarasa, watapangiwa shule katika awamu ya pili, kabla ya Februari 28, 2021, ndivyo anavyosema Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo.

Katika ufafanuzi wake, wanafunzi hao wataendelea kupangiwa shule kadri mikoa na halmashauri zitakavyoendelea kukamilisha ujenzi wa madarasa na madawati.

Hivyo, anawaagiza walimu na watendaji wa sekta ya elimu katika ngazi zote kuongeza bidii katika usimamizi na ufuatiliaji wa utoaji wa elimu, ili kufikia malengo ya elimu yaliyopangwa na serikali.

Anasema hayo wakati akitangaza wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza na kuitaja mikoa ya Kagera, Katavi, Lindi, Mtwara, Mwanza, Njombe, Ruvuma, Songwe na Tabora kuwa imeweza kupangia shule wanafunzi wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka ujao.

Nikirejea kwenye hoja yangu, si mara ya kwanza kuwapo kwa tatizo hili la uhaba wa madarasa, kwa kuwa limekuwa likijitokeza kila mwaka hivyo kuna haja ya kulitafutia ufumbuzi wa kudumu.

Uhaba wa madarasa kila mwaka si jambo jema ni wakati wa kulipatia ufumbuzi ili liwe ni jukumu la kila mmoja kwa nafasi yake na ikiwezekana ujenzi wa madarasa iwe ni ajenda ya kudumu, ili kupunguza kama si kumaliza tatizo hilo.

Ikiwezekana, ujenzi wa madarasa uwe ni mkakati wa kudumu ili kusaidia kumaliza tatizo hili linalojitokeza kila mwaka, ili kwamba wanafunzi wanapoanza kidato cha kwanza, ujenzi wa madarasa mengine uendelee kwa ajili ya mwaka unaofuata.

Wazazi na walezi, sekta binafsi ishirikishwe kwenye ajenda hiyo, ili wawe tayari kushiriki kikamilifu katika kuchangia nguvukazi yao au fedha, kwa ajili ya ujenzi madarasa, kwa kuwa wao ni wadau wakubwa wa elimu.

Ikumbukwe kuwa ushiriki katika shughuli za maendeleo ni jukumu la kila mwananchi, hivyo wana mchango mkubwa katika ujenzi wa madarasa, na ikiwezekana, tatizo hilo libaki kuwa historia.

Viongozi wa mikoa ambayo ina uhaba wa madarasa, si vibaya wakaenda kujifunza kwa wenzao, ambao wamefanikiwa kupangia shule wanafunzi wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka ujao.

Haina maana kwamba hakuna jitihada walizofanya, kwani zipo baadhi ya halmashauri ambazo wananchi wake wamehamasika, nguvukazi zao zinatumika kusomba maji, mchanga, mawe na mchanga kujenga madarasa.

Miongoni mwao ni wale wa Halmashauri ya Musoma, hasa Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, ambao wanashiriki ujenzi wa madarasa na hata shule mpya za sekondari za vijiji baada ya zile za kata.

Haipendezi kuona wanafunzi wakichelewa kuanza masomo kwa pamoja, kwa sababu ya uhaba wa madarasa, wakati uwezekano wa kuhamasisha wazazi na walezi katika ujenzi wa madarasa wa kutosha upo.

Kila halmashauri ichukulie ujenzi wa madarasa kama ajenda ya kudumu na siyo ya kuibuka kila mwaka, hali ambayo imekuwa ikisababisha baadhi ya wanafunzi kubaki nyumbani wakisubiri hadi madarasa yajengwe.

Utaratibu huo unawafanya baadhi ya wanafunzi kuwanyuma kimasomo, wakati wote ni wa kidato kimoja, hivyo wasaidiwe kuondokana na tatizo hilo kwa kuwekwa mkakati wa kuwa na madarasa ya kutosha.

Njia mojawapo ni kuufanya ujenzi huo kuwa ajenda ya kudumu, hasa kwa kuhakikisha madarasa muda wote na siyo kusubiri wanafunzi wachaguliwe kuingia sekondari ndipo pilikapilika za ujenzi zinaanza.

Mazoea hayo hayawezi kumaliza tatizo, badala yake wanafunzi wa kidato cha kwanza, kupishana katika kuanza muhula wa masomo kwa sababu ya kutoufanya ujenzi wa madarasa kuwa ajenda ya kudumu kwa taifa.

## HABARI KITAIFA

# Aliyefanya uganga kinyemela afungwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu mganga wa kienyeji Mazoya Makomango (36), kifungo cha miaka miwili jela au kulipa faini ya Sh. 100,000 kwa kosa la kufanya uganga bila kibali.

Mganga huyo mkazi wa Kijiji cha Chanika, mtaa wa Mtakuja, mkoani Geita alishindwa kulipa faini na kupelekwa jela.

Mfungwa huyo alifikishwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya, Samwel Maweda.

Hukumu hiyo ilitolewa jana baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka kwa mujibu wa hakimu.

Hakimu Maweda, alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kwa Makomango ili iwe fundisho kwake na kwa waganga wa kienyeji wengine wenye tabia kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na wakili wa serikali Janeth Kisibo, alipeleka mahakamani hapo mashahidi wawili na kielelezo kimoja ambavyo vilithibitisha kuwa mganga huyo alikuwa akifanya shughuli za tiba ya kienyeji bila kuwa na kibali.

Alisema polisi wa kituo cha Nyawilimilwa waliagizwa na mkuu wa kituo hicho kwenda kufanya msako kwa waganga wa kienyeji ambao wanafanya shughuli bila vibali.

Hakimu alisema baada ya kumkuta Makomango akiwa nyumbani kwake akifanya tiba za kienyeji bila kibali, aliulizwa na kukiri kuwa hakuwa nacho na kukamatwa.

Alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote na mshtakiwa umetiwa hatiani kwa kosa aliloshtakiwa nalo.

Pia mahakama hiyo ilimtaka ajitetee ili iweze kukupunguzia adhabu, naye aliomba ipunguzwe kwa kuwa ana familia inayomtegemea na kuangua kilio na kuomba Hakimu Maweda kuwapigia simu ndugu zake ili waje kumlipia faini ya Sh 100,000 mahakamani hapo.

Hakimu Maweda alitupilia mbali utetezi wa Makomango na kuamuru kwenda jela miaka miwili au kulipa faini ya Sh 100,000.

Awali akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Janeth Kisibo, alidai mahakamani kuwa Machi 10, mwaka huu, katika Kijiji cha Chanika Mtaa wa Mtakuja, wilaya ya Geita mshtakiwa alikutwa nyumbani kwake akifanya tiba za kienyeji bila kuwa na kibali, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Alikamatwa na polisi wa kituo cha Nyawilimilwa na kufikishwa mahakamani.

# 'Viongozi fichueni wahamiaji haramu'

**Na Ndalike Sonda,** SIMIYU

VIONGOZI wa serikali za mitaa, vijiji na kata mkoani Simiyu, wametakiwa kulinda amani kwa kuwafichua wahamiaji haramu wanaoweza kuhatarisha usalama wa nchi.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Simiyu, Mariam Mwanzalima, alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema viongozi hao wana nafasi ya kupata taarifa za wahamiaji hao mapema.

Alitaka kila kiongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi kata ahakikishe hakuna mtu anayefika eneo lake bila kupewa taarifa huku akiwataka wananchi kuwa wanalo jukumu la kushirikiana na viongozi kuwafichua wageni hao.

Pia, aliwataka wananchi wasiwakaribishe watu wasiowafahamu kwa kuwa wakikamatwa wanawahifadhi wageni hao wataadhibiwa kisheria.

Mwanzalima alisema Tanzania bila uhamiaji haramu inawezekana, hivyo kila mmoja ashiriki kuwafichua wanaojihusisha na kuwahifadhi.

"Cha msingi kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake ikiwamo kutoa taarifa kwa vyombo vya dola kuhusu kuwapo kwa watu wasiowafahamu," alisema ofisa huyo.

**Cha msingi kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake ikiwamo kutoa taarifa kwa vyombo vya dola kuhusu kuwapo kwa watu wasiowafahamu.**



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo (kushoto), Kamishna wa Polisi Zanzibar, Mohammed Hassan Haji, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Hamis na Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Johari Sururu, wakiangalia paa la moja ya nyumba za askari polisi zinazojengwa eneo la Finya, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, wakati wa ziara ya naibu huyo, kukagua miradi ya taasisi zilizopo chini ya wizara yake, jana Kisiwani Pemba. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI**

# Wizi, mauaji punda vyakithiri Kahama

**Na Moab Dominick,** KAHAMA

WAFUGAJI wa punda wamewaomba watendaji wa kata na wa vijiji vya maeneo wanapofugwa wanyama hao wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kusaidia kudhibiti wizi wa punda ambao sasa umekithiri.

Hatua hiyo inakuja baada ya wanyama hao kuibwa kwa kiwango kikubwa huku wengine wakiuawa na kuchunwa ngozi na mizoga yao kuachwa kuzagaa mitaani.

Walisema katika maeneo mbalimbali ya halmashauri ya Mji wa Kahama pamoja na Msalala kumekuwa na wizi wa punda kutoka kwa wafugaji na kupelekwa kusikojulikana na wengine kuchunwa ngozi hasa nyakati za usiku.

Hayo yalibainishwa juzi na baadhi ya wafuga punda katika maeneo ya Kagongwa na Mwendakulima katika mahojiano na Nipashe.

Walisema baadhi ya wanyama hao wanapelekwa katika machimbo madogo ya dhahabu kwa ajili ya kufanyishwa kazi.

Kadhalika, wezi hao wa punda pia wanawachuna ngozi na kuacha mizoga maporini ikizagaa hali ambayo inasababisha uchafuzi wa mazingira na kupoteza thamani ya mnyama huyo.

Katika Kata ya Kagongwa wafugaji hao walisema punda wanawasaidia kukua kiuchumi na kuinua kipato chao wanapowatumia katika kazi za ujenzi pamoja na kuchota maji.

Mmoja wa wafugaji hao, Boniphace Protace, alisema wizi wa punda katika maeneo yao ni mkubwa na kuongeza kuwa ni vyema watendaji wa kata na vijiji washirikiana kuuzuia.

Protace aliziomba halmashauri hizo kufikiria kutunga sheria ndogo ambazo zitawabana hasa wezi hao pamoja na wafugaji ambao wamekuwa wakiwatendea ukatili mkubwa wanyama hao.

Alisema pamoja na kuwapiga mapanga na kuwatumia bila ya kuwatibu, wanapokufa huacha mizoga ikiwa inazagaa barabarani na maporini huku ikitoa harufu mbaya.

Kwa upande wake Ofisa wa Shirika la Kutetea ustawi wa Wanyama (TAPO), wilayani Kahama, Master George, alisema shirika hilo limekuwa likitoa elimu kuhusu mnyama huyo kwa wafugaji.

George alieleza kuwa TAPO inatoa elimu kwa wafugaji hasa wa punda kuwalinda na kuwatibu na kuzuia kuwapiga wanyama kazi hao.

Akizungumzia wizi George alisema kuna baadhi ya mawakala wa raia wa mataifa fulani (jina tunalo) wanaopita vijijini kwenye wafugaji wa wanyama hao na kuwadanganya kwa kuwapa kiasi kidogo cha fedha na hivyo kuwachukua.

Alisema wanawapeleka kwenye kiwanda cha nyama kusindikwa kitoweo.

## HABARI KITAIFA

# Jeshi la Polisi lanasa watuhumiwa 683 uhalifu

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

JESHI la Polisi limewakamata watuhumiwa 683 kwa makosa mbalimbali mkoani hapa katika operesheni iliyochukua wiki tatu katika wilaya za mkoa huo.

Mkuu wa Operesheni Maalumu wa Jeshi la Polisi Tanzania Kamishna Mwandamizi wa Jeshi wa Polisi (SACP) Mihayo Msikhela, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema miongoni mwa watuhumiwa hao 277 wamefikishwa mahakamani na kuhukumiwa, 255 kesi zao zinaendelea na watuhumiwa 42 wako katika uangalizi wa polisi baada ya kutokuwapo kwa ushahidi madhubuti.

SACP Msikhela alisema baadhi ya vielelezo vilivyokamatwa ni silaha aina ya gobore, mapanga, meno ya tembo mawili, pikipiki 34, magodoro 10 na simu za mkononi nne.

Vitu vingine ni vyuma vya reli viwili, runinga za aina mbalimbali 19, mfano wa sare za majeshi mbalimbali ya ndani na nje na pombe haramu ya gongo lita 408.

Aliongeza kuwa miongoni mwa watuhumiwa hao wamewakamata raia wa nje kabila Mhutu akiwa na aina mbalimbali za mfano wa sare za polisi na majeshi mengine.

SACP Msikhela alisema mtuhumiwa huyo akikamatwa baada ya askari polisi kumwona amevaa sare ambazo zinafanana na za polisi, lakini mshono wake ni tofauti.

Alisema baada ya kupekua begi alililokuwa amebeba, walikuta sare zinazotaka kufanana na za Jeshi la Wananchi na nyingine zinafana na za majeshi ya nje.

SACP Msikhela alisema katika operesheni hiyo ya kuanzia Desemba 7, wamebaini kuwa magenge yanayojihusisha ni uvunjaji, uporaji na wizi ni vijana ambao umri wao ni kuanzia miaka 15 hadi 21.

Alisisitiza Jeshi la Polisi litaendelea kufanya operesheni na misako ya mara kwa mara kwa kushirikiana na raia wema ili kukomesha uhalifu mkoani Tabora.




Ofisa Programu Msaidizi wa Projekt Inspire, Kelvin Joseph, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, kuhusu kambi ya siku tano ya wanafunzi kutoka shule 70 za umma na binafsi nchini inayoanza leo jijini Tanga. Mradi huo unahamasisha vijana kupenda masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM). Kulia kwake ni Edwin Mshahara. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Madereva wafunguka kupelekwa mochwari

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MADEREVA wilayani Tunduru wamepokea kwa hisia tofauti kauli ya Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani humo, cha kuandaa utaratibu wa kushirikishwa kwenda hospitalini kuangalia miili ya watu waliopoteza maisha na majeruhi wa matukio ya ajali, ikiwa ni lengo la kupunguza matukio ya ajali.

Wamesema hatua hiyo haitasaidia kwa kuwa kuona majeruhi au watu waliopoteza maisha kwa ajali hakuwezi kubadilisha tabia za madereva.

Juzi Kamanda wa Usalama Barabarani wilayani Tunduru, Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Anosisye Mwaipopo, alisema wanaandaa utaratibu wa kuwapeleka madereva mochwari kuangalia miili ya watu waliopoteza maisha, majeruhi wa ajali ili kushuhudia walivyoumia.

Wakizungumza na Nipashe, miongoni mwa madereva hao Oweni Makochela, ambaye katika maelezo yake alisema kuwa tabia ya dereva anayependa kuendesha chombo cha moto haiwezi kubadilishwa kwa yeye kwenda kuona majeruhi wa ajali hospitalini.

Dereva mwingine, Mahamudu Katomondo alisema uwezekano wa ajali kupungua au kutopungua kwa matukio ya ajali kutategemea mapokeo ya elimu hiyo kwa wahusika.

Majidi Kasimu ambaye ni dereva pikipiki alisema madereva bodaboda hushtuka wakati wanapoona tukio, lakini baada ya kuondoka eneo la ajali hujisahau na kuendelea kuvunja sheria za barabarani.

"Huwa inauma na kushtua pale tu unapoona au kukutana na tukio la ajali, lakini baada ya kuondoka eneo la tukio huwa tunajisahau na mwendo tunaongeza kama kawaida," alisema Kasim.

Baadhi ya madereva walilipongeza Jeshi la Polisi kwa kubuni utaratibu huo na kuliomba kutilia mkazo katika usimamizi wa sheria za usalama barabarani, kutoa elimu kwa madereva.

# Vijana waonywa kuhusu injili ya kupotosha

**Na Issack Matogoro,** MWANZA

VIJANA nchini wamepewa tahadhari kuacha kupokea mahubiri potofu bila ya kuyafanyia uchambuzi makini na wa kina kwa kuwa hutolewa na watu wenye lengo la kugeuza neno la Mungu kuwa kitega uchumi.

Tahadhari hiyo imetolewa jana mjini Mwanza katika mkutano wa Kambi ya Vijana wa Kanisa la Zion Gospel Assembly (ZGA) Tanzania, ambao unahudhuriwa na vijana wasiopungua 350 nchini.

Askofu wa kanisa hilo, Elly Mpule, katika ufunguzi wa mkutano huo alisema, baadhi ya vijana nchini huamini kuwa wameokoka kwa kutangaziwa na wahubiri wanaofanya biashara ya neno la Mungu na kuligeuza kitega uchumi bila wenyewe kuelewa maana ya kuokoka.

Askofu Mpule kutoka Shinyanga alisema kutokana na hali hiyo baadhi ya vijana huchanganyikiwa na kuamini kuwa wameokoka baada ya kufahamu kuwa uokovu ni hatua itokayo ndani ya roho ya mtu na siyo tangazo kutoka kwa wahubiri ambao wametapakaa nchini.

Mkutano huo unafanyika huku mahubiri ya injili zenye tafsiri tofauti yakiwa yameenea sehemu mbalimbali kupitia mikusanyiko mbalimbali na vyombo.

Mchungaji Victor Rushoneza kutoka Serengeti, akichangia hoja hiyo, alisema siku hizi vijana wanaoamini kuwa wanaweza kurithi uokovu toka kwa wazazi wao wakati kitendo hicho kinatakiwa kutoka katika roho ya muhitaji wa kuokoka.

Alisema mahubiri ya injili ya kupotosha yamesababisha vijana na watu wazima kuamini kuwa matumizi ya vitambaa, asali, mafuta na maji vinavyouzwa na baadhi ya wahubiri vinaweza kutibu maradhi jambo ambalo halina ukweli.

Katika tukio hilo pia katibu wa kanisa hilo, Mchungaji Lazaro Maalim, kutoka Serengeti alisema baadhi ya vijana wana mawazo ya kutegemea urithi kutoka kwa wazazi wao badala ya kuandaa na kubuni mikakati ya kujitegemea kwa ajili ya maisha yao.

Mkutano huo ambao hufanyika mara moja kila mwaka unalenga kuwaandaa vijana kuwa tayari kujenga uwajibikaji wa ujenzi wa kanisa na nchi nzima kwa ujumla.

**Mkutano huo unafanyika huku mahubiri ya injili zenye tafsiri tofauti yakiwa yameenea sehemu mbalimbali kupitia mikusanyiko mbalimbali na vyombo.**

HABARI KITAIFA

## Simbachawene asisitiza kuitunza amani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawane, amewataka Watanzania kutunza amani iliyopo nchini na pia kuenzi misingi ya maadili mema iliyoachwa na waasisi wa taifa.

Amesema amani na upendo huanzia katika familia, katika kipindi cha Sikukuu ya Krismasi familia zinajenga upendo na amani, iwe pia katika kujenga taifa.

Alisema hayo katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria wa Rozali Pwaga, Jimbo la Kibakwe, wilayani Mpwapwa, juzi, wakati familia ya marehemu mzee Simbachawene ilipowaombea marehemu mbalimbali wa ukoo huo.

"Familia ziishi kwa upendo, kushirikiana, kusameheana, kupendana, kuwa na amani, hivyo familia zinapoungana zinaunga jamii na zinajenga upendo ndani ya taifa, kila mtu achukue nafasi yake katika familia yake ili tuweze kujenga taifa," alisema Simbachawene.

Pia Waziri Simbachawene alisema, mwaka 2020 unaishia ikiwa nchi imepitia katika matukio makubwa, hata hivyo imebaki salama, matukio hayo ni ugonjwa wa corona, pia uchaguzi mkuu umemalizika ukiwa wa huru na amani, hatua zote hizo ni kumshukuru Mungu kwa taifa kuvushwa salama.

"Nchi mpaka sasa ipo salama, dunia imepigwa na corona, lakini sisi Tanzania tupo salama, tumepita katika uchaguzi mkuu umeisha salama, uchaguzi haukosagi kelele, hata Marekani kuna kelele, vuo wameendelea na ndio taifa kubwa duniani," alisema Simbachawene.

Pia, aliwataka madereva wa vyombo vya moto hasa bodaboda kuwa makini barabarani kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, kuepuka ajali.

"Kuna kupungua sana kwa hali ya ajali nchini kwa miaka mitano iliyopita mpaka sasa, mwaka 2017 kiwango cha ajali kilikuwa 9,250, lakini tangu Januari mpaka Novemba, mwaka huu ajali zilikuwa 1,602 hii kwasababu wananchi wanaendelea kufuata sheria za usalama barabarani, lakini pia askari polisi, kitengo cha trafiki wamefanya kazi vizuri, kuhakikisha wanaendelea kudhibiti ajali," alisema Simbachawene.

# Wawili wapoteza maisha kwa kukosa huduma kituo cha afya

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WATU wa wawili akiwamo mtoto mchanga wamepoteza maisha kwa kukosa huduma katika Kituo cha Afya Lunguya, Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama, kutokana na wahudumu wa kituo hicho kutokuwapo kazini.

Mtoto huyo alipoteza maisha juzi akiwa tumboni mwa mama yake baada ya mama huyo kukosa huduma huku mgonjwa mwingine akikumbwa na umauti wakati akisubiri matibabu katika kituo hicho.

Hali hiyo ilibainika baada ya Mbunge wa Jimbo la Msalala, Iddy Kassim Iddy, kufanya ziara ya ghafla katika kituo hicho na kukuta hali hiyo ambayo haikumfurahisha na kukerwa na huduma inayotolewa kituoni hapo.

Akiwa katika kituo hicho, Mbunge Iddy alipiga simu kwa mkuu wa kituo, ili kupata ufafanuzi wa kutokuwapo kwa wahudumu kituoni.

Hata hivyo, mbunge huyo alisema kiongozi huyo alishindwa kutoa majibu kuhusu tukio hilo lililosababisha kupoteza maisha kwa watu hao wawili.

**Sasa tunaweza kufanya shughuli mbalimbali katika maeneo tofauti, tunaishukuru sana TCC na tunawaomba wasiishie hapo kwani bado msaada wao unahitajika.**

Mbunge huyo aliamua kuchukua jukumu la kuwabeba wagonjwa wote waliokuwapo katika kituo hicho kwenye gari lake maalumu alilonunua kwa ajili ya kuwabeba wagonjwa jimboni na kuwapeleka katika maeneo mengine kupata huduma.

Alisema kuwa alilazimika kuwachukua wagonjwa hao na kuwapeleka katika kituo cha afya jirani cha Chella kwa ajili ya kupatiwa matibabu ya haraka baada ya kukosa huduma katika kituo cha Lunguya.

Kwa upande wao, wananchi wa Kata ya Lunguya pamoja na wagonjwa waliokuwapo katika kituo hicho, walitoa malalamiko yao kwa mbunge huyo kuwa tatizo la wahudumu wa kituo hicho kutokuwapo kazini wakati wa kazi limekuwa ni sugu pamoja na kuwa na lugha chafu kwa wagonjwa.

Walisema kuwa mbali na kuwa na changamoto hiyo pia kumekuwa na huduma duni hali ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa wagonjwa kuhama katika eneo hilo na kwenda kutafuta matibabu katika zahanati za jirani.

Mbunge Iddy aliahidi kukutana na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Msalala, Ernest Nyambogo, kutatua tatizo la kituo hicho na matatizo mengine katika Jimbo la Msalala kwa maslahi ya wananchi wa jimbo hilo.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Msalala, Nyambogo, alipotakiwa kuzungumzia tatizo la kituo cha afya cha Lunguya, alisema mtoa huduma katika kitengo cha damu salama kituoni hapo ni mmoja na siku ya tukio hakuwapo.

Nyambogo alisema kuwa kati ya wagonjwa hao waliokwenda kutafuta damu katika kituo hicho cha afya Lunguya, mmoja wao kundi lake la damu lilikuwa halipo katika kituo hicho mpaka katika kituo cha afya cha Chella na kuongeza kuwa tatizo lingineni uchache wa watumishi pamoja na dawa.



Mkurugenzi wa Mipango, Utafiti na Maendeleo ya Masoko kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania, Muyengi Zakaria, akimkabidhi cheti Meneja Mwandamizi wa Bima wa Benki ya NMB, Martin Massawe, ikiwa ni kutambua mchango wa NMB katika sekta ya bima nchini, kwenye mkutano wa wadau wa bima uliofanyika mwishoni mwa juma. Wengine ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam, Khamis Suleiman (katikati). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndaki achangia vifaa ujenzi shule sekondari, msingi

**Na Happy Mollel,** MASWA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amechangia vifaa vya ujenzi kwa ajili ya Shule ya Sekondari Mwang'honoli na nyumba tatu za walimu katika Shule ya Msingi Jihu, Wilaya ya Maswa, mkoani Simiyu.

Mashimba ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, amekabidhi vifaa hivyo katika mikutano ya hadhara iliyofanyika jana kwa nyakati tofauti katika kijiji cha Mwang'honoli na Jihu.

Katika mkutano wake wa awali Kijiji cha Mwang'honoli, alikabidhi vifaa vyenye thamani ya Sh. 2,450,000 ambavyo ni mabati, mbao, misumari na mifuko 60 ya saruji na kueleza kuwa lengo ni kuhakikisha shule hiyo inakamilika kwa wakati Januari mosi, mwakani ili isajiliwe na kufunguliwa kwajili ya kuanza rasmi masomo ya kidato cha kwanza.

Alisema kukamilika kwa shule hiyo kutasaidia kupunguza umbali kwa wanafunzi wa kata hiyo.

"Wanafunzi wenu wanasafiri umbali mrefu kutoka katika Kata yenu ya Mwang'honoli hasa wanaochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari, tukikamilisha ujenzi wa shule hii kwa wakati hili tatizo litaondoka maana watasomea hapa hapa," alisema Mashimba.

Waziri hiyo ameeleza kusikitishwa na kitendo cha uongozi wa kata hiyo kushindwa kusimamia kikamilifu ujenzi wa shule hiyo wakati vifaa vyote vya ujenzi vikiwapo na kumwagiza Mkuu wa wilaya hiyo, Aswege Kaminyoge, kuhakikisha kuwa shule inakamilika ifikapo Januari mosi, mwakani.

Katika mkutano wake wa hadhara katika kijiji cha Jihu aliwapongeza wananchi wa kijiji hicho kwa uamuzi wao wa kuamua kujenga nyumba tatu za walimu ili kupunguza tatizo la upungufu wa nyumba za kudumu za walimu hao.

Alisema katika kuunga juhudi zao ameamua kuchangia vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. 2,242,000 pia alijitolea kulipa gharama za fundi ambaye ataezeka nyumba hizo.

# Meya awatangazia kiama wenye harufu ya ufisadi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MEYA wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, amewaonya wafanyakazi mafisadi waliozoea kuchuma fedha na kuiacha manispaa hiyo bila maendeleo kuwa hatawavumilia.

Alisisitiza kuwa hatakuwa na mzaha kwa watumishi wazembe, ambao wamezoea kuchuma fedha kwenye mji huo na kisha kuondoka na kuuacha bila maendeleo, akiwaambia wakae mguu sawa.

Nkulila alitoa onyo hilo juzi kwenye mkutano wa kufunga mwaka wa Shirika la kiraia la UDIDA, linalojishughulisha na ustawi wa jamii, uliojadili changamoto za mwaka huu pamoja na kupanga mikakati ya utendaji kazi mwakani.

**Manispaa ya Shinyanga ina baadhi ya watumishi wazembe, lakini mabingwa wa kuchuma fedha na kuondoka.**

Alisema Manispaa ya Shinyanga ina baadhi ya watumishi wazembe, lakini mabingwa wa kuchuma fedha na kuondoka.

Aliwaonya kuwa ndani ya miaka mitano ya uongozi wake atawanyoosha waajiriwa wa namna hiyo.

"Fedha zipo za kufanyia maendeleo, lakini tunavurugwa na baadhi ya watumishi ambao ni wazembe wanaoifanya manispaa yetu kuwa sehemu ya kuchuma fedha kisha kuondoka. Waambieni wakae mguu sawa sitakuwa na mzaha," alisema Nkulila.

"Kwenye mchakato wa kuomba nafasi ya umeya, tulikuwa watu wanne, lakini kamati kuu ya CCM ilichuja likarudi jina langu, hivyo sitamwangusha Rais John Magufuli, kutokana na kuniamini, lazima niache alama ya maendeleo hapa Shinyanga tutaonana wabaya,"aliongeza.

Aliahidi ushirikiano na wadau wa maendeleo ambao wanafanya shughuli zao kwenye manispaa hiyo na kuitaka asasi hiyo ya UDIDA, ifanye kazi kwa kutimiza malengo yao ikiwamo kuhudumia jamii pamoja na kuwa na nidhamu ya fedha kwenye mipango yao ndipo wataweza kufika mbali.

Mkurugenzi wa UDIDA Jasson Kyaruzi, alisema katika mipango yao utendaji kazi mwakani wataendelea kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine, kutoa huduma ya misaada mbalimbali ndani ya jamii hasa yenye uhitaji kama ilivyofanya mwaka huu.




Mshindi wa nne wa promosheni ya Vodacom Tanzania, Shangwe Shangwena, Regina Kashmir, mkazi wa Moshono jijini Arusha, akifungua mlango wa gari mpya aliyojishindia kwenye promosheni hiyo juzi. Anayeshuhudia kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongosi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UWT Pangani wafurahia miradi ya maendeleo

**Na Steven William,** PANGANI

KATIBU wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, Catherine Makungwa, amesema wamefurahishwa na utendaji kazi wa Rais John Magufuli kwa kupeleka miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani humo.

Alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisi kwake, wilayani Pangani jana.

Makungwa alisema utendaji kazi wa Rais Magufuli umewaridhisha viongozi wa Jumuiya hiyo, wanachama wa CCM na wananchi wa Pangani kwa kuwabana mafisadi na kuokoa fedha za serikali.

Alisema utendaji kazi wa Rais Magufuli unaonekana kwa wakazi wa Pangani baada ya kuleta miradi mbalimbali ya maendeleo ukiwamo wa barabara.

Pia, mradi wa ujenzi wa daraja la Mto Pangani na barabara ya kutoka Tanga Mjini kuelekea wilayani Pangani mpaka Sadani kwa kiwango cha lami unaendelea kwa kasi na itafungua uchumi wa wilaya hiyo.

Alisema sasa wanasubiri mradi mkubwa kutoka Mto Pangani ambao ndio utamaliza tatizo la maji katika wilaya ya Pangani, Muheza, Korogwe na Handeni.

Mwenyekiti wa UWT wilayani Pangani, Hadija Mvaa, alisema Rais Magufuli ameleta miradi ya umeme wa REA na kwamba vijiji vya wilaya hiyo vimepata huduma hiyo muhimu kwa shughuli za maendeleo.

Kwa upande wake mjumbe wa kamati ya siasa CCM Wilaya ya Pangani, Amina Mwaopea, alisema Rais Magufuli amewasaidia wanawake kupata mikopo ya asilimia kumi ya halmashauri na ameleta miradi ya afya na elimu na hivi sasa wananchi wameanza mpango wa ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari na kutengeneza madawati na ujenzi wa matundu ya vyoo.

# Mahakama yafuta kesi ya kunajisi kwa kukosa ushahidi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa wa Wete imeliondoa shauri lililokuwa likimkabili mtoto mwenye umri wa miaka 16, mkazi wa Bubujiko Wete, aliyetuhumiwa kumnajisi mtoto wa kiume wa miaka mitano baada ya mashahidi kutofika mahakamani.

Hukumu hiyo, imekuja baada ya Wakili ya Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Mohamed Said Ali, kudai kuwa, shauri hilo lipo muda mrefu mahakamani bila ya kusikilizwa mashahidi.

Alidai kuwa, ingawa kesi hiyo ipo kwa ajili ya kusikilizwa, lakini kila wakiitwa mashahidi mahakamani hapo hawafiki, licha ya kupelekewa barua ya wito na kuiomba mahakama kuliondoa shauri hilo.

"Mheshimiwa hakimu shauri hili lipo kwa ajili ya kusikilizwa mashahidi, lakini kila wakiitwa, hawafiki hivyo tunaiomba mahakama hii kuliondoa shauri hili kwa kutumia kifungu cha103 (a) cha Sheria ya mwenendo wa jinai namba 7 ya mwaka 2018," alidai wakili huyo.

Alidai kuwa, katika shauri hilo walisikilizwa mashahidi wawili pekee, ingawa wengine hawakutaka kufika mahakamani na kuona bora kwa mahakama ikaliondosha.

Hakimu wa mahakama hiyo, Abdalla Yahya Shamhun, alikubali ombi la upande wa mashtaka na kusema kuwa mahakama imeliondoa shauri hilo.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, mtuhumiwa huyo alitenda kosa Januari 13, mwaka huu, majira ya saa 11:50 za jioni katika eneo la Mtemani, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa kuwa, mtuhumiwa huyo alimnajisi mtoto huyo mwenye umri wa miaka mitano, jambo ambalo ni kosa kisheria.

Kufanya hivyo ni kosa kinyume na kifungu cha 115 (1) cha Sheria ya Adhabu nambari 6 ya Mwaka 2018 Sheria ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kesi hiyo yenye kumbukumbu namba JV2/2020 kwa mara ya kwanza ilianza kusikilizwa katika Mahakama ya Mkoa Wete, Machi 10, mwaka huu, ingawa kwa kipindi chote hicho upande wa mashtaka umekuwa ukitoa hati za wito kwa mashahidi na kushindwa kufika mahakamani bila kutoa sababu za msingi.

Nipashe
# TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Jumanne Desemba 29, 2020



Ukurasa 14

**KERO ZILIZOUDHI WENGI**



Ukurasa 12

**NDOTO YA WANAMAZINGIRA**



Ukurasa 13

KWA HERI MWAKA 2020

TEKNOLOJIA

**NA MWANDISHI WETU**

# DOZI YA KUFANIKIWA NA 'KUPAA' KIMAISHA 2021

MAISHA ni mapambano na unahitaji mbinu za medani. Ambao ni ujanja unaotumiwa na majeshi vitani kuwashinda maadui.

Unapoingia mwaka mpya, Tanzania imejaa mambo mengi, lakini 'presha' kubwa iko kusaka na kupata pesa ili kuwa tajiri au mwenye maisha bora.

Mwaka unapomalizika kuna watu walitumia mbinu za kihalifu kama kuua hata kujeruhi na kupora, kufuata maelekezo ya waganga wa kienyeji waliowaambia waue jamaa zao, wapo walioiba kwa njia ya simu, kuna waliotapeli, kula rushwa na kutumia kila aina ya uovu ili wafanikiwe. Jiulize wewe ulifanya nini?

Lakini, kuna wengi ambao hawakufanikiwa kuwa mamilionea zaidi ya walipoteza wakati na mali, katika mwendelezo huo wa kusaka pesa wapo waliokufa. Vile vile kuna waliopata utajiri kwa njia za uhalifu ambao mwaka unapokwisha hawana furaha, unaweza kuwa miongoni mwao.



Inawezekana tangu alfajiri hadi usiku wa manane watu hawapati muda wa kupumzika, kuomba Mungu, kula na hata kuzungumza na wanafamilia au jamaa zao kisa wanasaka fedha na wako 'bize' muda wote na wanachowaza wakati wote ni namna ya kupata pesa zaidi ili kuwa na maisha bora na utajiri.

Ni vyema kufanyakazi kazi kwa bidii, kujituma kwa juhudi zote na nguvu na kuondoka vijiweni kwa lengo la kujipatia mafanikio, lakini ujiulize ninachofanya kinaendana na taratibu za kiubinadamu na kuheshimu maisha ya wengine?

Kwa ujumla huu ni wakati wa kujiuliza tuliweka malengo ya kufanyakazi kwa bidii na hata kutumia mbinu hizo zikiwamo za kiuhalifu ili tupate nini? Ama ilikuwa ni kupata pesa au utajiri au kuna la zaidi. Vipi kuhusu kuwa na furaha katika maisha yetu?

Mbali na kuwa na maisha bora ni burudani kuwa na fedha unapomaliza mwaka jiulize, tunapofanyakazi hizo kwa bidii na juhudi tumeongeza upendo katika familia zetu, ndugu zetu au tunazidi kuwa mbali nao? Hili limekufanya mama kuwa karibu na furaha zaidi na watoto wako?

Au umekuwa 'bize' hata watoto wako kutoonana na wewe kwa mwaka wote? Wamebakia mikononi mwa watumishi wa ndani au wanalelewa na wazazi wako mkoani na wafanyakazi wakati wewe uko Dar? Au umewakimbiza wakakae shule za bweni wakiwa na miaka mitatu ili ufanikiwe kwenye 'mishemishe' kusaka pesa?

Iwapo umechemka panga 2021 kuwasikiliza watoto, kuwauliza habari za masomo, kuwahudumia siyo kuwahamishia shule za bweni au kuwapeleka kwa wazazi na ndugu vijijini au mikoani.

**MALENGO/TUNZA AFYA**

Sawa, mafanikio ni pamoja na kufanya kazi kwa bidii, lakini unajiwekea malengo au unaamua kusaka fedha kila siku kama kichaa bila kujua unataka upate kiasi gani na ufanye nini? Usitake kufanya kazi mwaka mzima na kukurupuka bila kuwa na lengo la kutimiza. Angalia, tembea na malengo na ukumbuke afya yako.

Iwe umejiajiri au umeajiriwa pamoja na biashara zako nyingi na kupata kipato unachotamani kumbuka mwili wako unahitaji kupumzishwa na kufanyiwa ukarabati kwani hata injini na mitambo inapumzishwa kufanyiwa 'service'. Usijisahau.

Zama hizi utulivu wa akili umekuwa tatizo kubwa kiafya. Wengi wanaofanya kazi wakiwa na msongo wa mawazo uliopitiliza, hofu na hata kuchanganyikiwa. Lazima kuupumzisha mwili ikibidi kuufanyia uchunguzi wa kiafya au kuukarabati ili ufanyakazi kwa ufanisi zaidi 2021.

Kumbuka ukiwa na msongo wa mawazo unapungukiwa na uwezo wa kufikiri kikamilifu na kufanyakazi kwa bidii ili kutimiza malengo yako.

**UNAJIPA RAHA MWENYWE**

Unapoingia 2012 , penda kufurahia maisha baada ya kazi ngumu, kaa na familia yako, wazazi na marafiki, angalia runinga nenda kwenye ibada, omba, sifu, abudu itakusaidia kupunguza msongo wa mawazo.

Jua maendeleo ya watoto wako wa ndugu zako, sikiliza matatizo yao na kujua namna ya kuwasaidia.

Wengi wamekuwa kazi ni wao ni kazi ili kutafuta pesa lakini hata wanapozipata wanakosa kufurahia. Maisha yanakuwa hayana maana. Hawana wa kuwaeleza hofu wala machungu yao.

Usikae na sonona nenda kwa wataalamu wa saikolojia, washauri nasaha. Ongea na wazazi wako lakini pia familia, tafuta amani ya roho.

**HUJUI YA KESHO**

Samehe na kuacha vinyongo na kubeba watu rohoni ati fulani hamsalimiani na umeweka fundo moyoni, vuka mwaka na furaha kwa kujua kuwa bila raha na amani rohoni ni vigumu kufurahia fedha unazosaka kwa nguvu zote.

Cha muhimu wakati unaanza mwaka wa 2021 kumbuka kuwa maisha ukiwamo kupata utajiri, kula na kunywa unavyotaka, kuwa mwenza unayempenda na familia ya kuringia yote yana mwisho.

Kwa hakika hakuna anayejua lini yanamalizika. Hata ukijaribu kupiga hesabu za harakaharaka kujua namna ulivyofika kwenye umri ulionao leo huna jibu unabaki kushangaa.

Vivyo hivyo maisha hayana 'garantii' siku yoyote na wakati wowote pumzi inakata usiache kusali na kumuomba Mola. Angalia hivi karibuni ilizuka COVID -19 watu wengi wakafariki dunia hata kama wana pesa kiasi gani, maelfu ya watu Ulaya wakiwamo mabilionea waliaga dunia.

Sasa hebu jiulize unafanya kazi na kupambana usiku na mchana mwenyewe ukijifariji kwa kusema nitaanza kuomba na kumkumbuka Mungu baadaye. Unafungua duka kuanzia Januari mosi hadi Desemba 31, Jumapili mpaka Jumapili, huna ibada wala shukrani kwa Mungu. Unajua kesho itakuwaje?

Tunawashukuru kwa kusoma Nipashe 2020, tukutane tena wiki ijayo Jumanne Januari 6, 2021. Heri ya Mwaka Mpya msomaji wetu.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# NDOTO YA WANAMAZINGIRA

## ■2021 ulete Baraza la Rufani



Mashauri ya miradi mikubwa ya kuchimba madini inahitaji Baraza la Rufani la Mazingira. **PICHA: MTANDAO**

MABADILIKO ya tabianchi ni moja ya changamoto isiyo na majibu, inayotikisa dunia zama hizi. Kila taifa linalalamikia uharibifu wa mazingira unaoleta athari nyingi kwa raia wake. Wapo wanaolalamikia joto kali, vimbunga, ongezeko kina cha bahari, ukame unaotisha, magonjwa na hivyo kila nchi kuweka mikakati madhubuti ya kutunza na kusimamia mazingira yake.

Tanzania haijabaki nyuma katika kutekeleza wajibu huo wa kulinda mustakabali wa Watanzania na mazingira yao, bunge lilitunga Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 (Sheria ya Namba 20 ya mwaka 2004.), ambayo kifungu cha 204, kinaanzisha Baraza la Rufani za Mazingira.

Mwanasheria wa asasi ya kiraia ya Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Clay Mwaifwani, anasema, Baraza la Rufani la Mazingira ni chombo halali chenye mamlaka ya kupokea rufani, iwapo yeyote amegadhibika na maamuzi ya waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa mazingira.

Maamuzi yanaweza kuhusu kuwekwa au kutowekwa sharti fulani lenye kuhusiana na usimamizi wa mazingira, ukomo au kizuizi kwa mujibu sheria ya mazingira au kanuni zake na pia kutoa ufafanuzi wa suala lolote lile lihusulo sheria hiyo.

Pengine hii ni mara ya kwanza kwa wengi kusikia kuhusu Baraza la Rufani la Mazingira, chombo chenye mamlaka ya kimahakama ya kusikiliza shauri la kimazingira na kulitolea uamuzi.

Karne ya 20 imeshuhudia uanzishwaji wa mabaraza ya namna hiyo sehemu mbalimbali duniani akisema, sehemu ya 17 ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inaainisha mamlaka na majukumu ya baraza hilo.

Inayataja kuwa ni pamoja na kuendesha mashauri kwa mfumo wake, nguvu yake ya kufanya maamuzi, vyanzo vya mapato, kinga za watendaji wake na rufani kwenda Mahakama Kuu.

Licha ya uwingi wa vifungu vyenye kuelezea Baraza la Rufani za Mazingira, kinachoweza kuonekana kama ni jambo la kushangaza ni kwamba, Tanzania haina chombo hicho muhimu kinachohitajika kulinda maliasili muhimu za nchi.

Yapo mambo ambayo sheria haiyasemi au inayasema kwa uchache mfano, mabadiliko ya tabianchi, lakini Baraza la Rufani za Mazingira sheria imelijadili kwa upana wake na kulipa Baraka zote.

**LIKO WAPI?**

Swali linaloulizwa na wengi ni hili ni kwanini baraza hilo halijaanzishwa hadi sasa? Licha ya uwepo wa mahakama za kawaida zinazopokea mashauri kila siku, zikiwamo kesi za kimazingira, bado kuna ulazima na umuhimu mkubwa wa kuwa na baraza mahususi lenye mamlaka ya kusikiliza masuala ya mazingira na kuyatolea maamuzi pasipo kuingiliwa na chombo kingine chochote, anasema Mwaifwani.

Mahakama za kawaida huwa na mrundikano mkubwa wa kesi mbalimbali, uwingi wa mashauri hayo ni kikwazo kikubwa kwa utatuzi na kushughulikia masuala ya kimazingira kwa wakati.

Inawezekana wakati mwingine miradi mikubwa ya uwekezaji husimama kusubiri maamuzi ya mahakama juu ya shauri la kimazingira mfano tathmini ya athari za kimazingira, kwa mujibu wa Mwaifwani.

Mbali na suala la muda, changamoto nyingine kubwa kwenye mahakama za kawaida ni uwingi wa vikwazo vya kisheria.

Hizi ni pamoja na sheria zenye kueleza taratibu kama vile sheria ya mwenendo wa mashauri ya madai zina vipengele vingi vinavyoweza kuleta mkanganyiko iwapo mlalamikaji hakuvifuata ipasavyo. Vigingi vya namna hiyo havigusi kiini cha shauri, lakini vinaweza kumaliza kesi bila kiini cha mgogoro kusikilizwa.

> “ Inawezekana wakati mwingine miradi mikubwa ya uwekezaji husimama kusubiri maamuzi ya mahakama juu ya shauri la kimazingira mfano tathmini ya athari za kimazingira, kwa mujibu wa Mwaifwani.

Mwaifwani anaona kuwa wakati mwingine majaji au mahakimu wa mahakama za kawaida hukosa uelewa kuhusu masuala ya mazingira.

Wanapokosa utaalamu mahususi wa mambo ya mazingira, kama wapo kwenye mahakama za kawaida huyatizama kwa namna nyepesi na wakati mwingine masuala muhimu ya kiikolojia hayapewi uzito unaostahili hivyo kukwamisha jitihada za uhifadhi wake.

Kwa kutambua umuhimu wa maendeleo endelevu (dumivu), Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, imeanzisha chombo hicho na kifungu cha 204, kuainisha kuwa wafanya maamuzi wa baraza watatakiwa kuwa na elimu, uzoefu na weledi kwenye masuala ya sheria na mazingira. Wafanya maamuzi wa aina hiyo ni suluhisho muhimu kwa manufaa ya vizazi vijavyo ya mazingira ya Tanzania, anasema mwanasheria huyo.

Anaungwa mkono na mwanasheria Baraka Thomas kutoka LEAT anayesema kutokuanzishwa kwa baraza hilo ni kikwazo cha kiutawala kwani bunge lilikwisha kufanya kazi yake kwa kuandaa vitendea kazi yaani sheria inayoanzisha chombo hicho.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 pia, pia kifungu cha 230, inampa Mamlaka Waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa mazingira kutunga kanuni zitakazowezesha utekelezaji bora wa sheria.

Anaongeza: “Ni jambo la kufaa na kupendeza sana iwapo nafasi hiyo ingetumika kutunga kanuni za usimamizi na uendeshwaji wa mambo yote yahusianayo na Baraza la Rufani la Mazingira, ili mashauri yote yaanze kusikilizwa mbele ya chombo maalumu chenye watendaji wenye utaalamu na uzoefu mahususi wa sheria na mazingira.” Anasema.

Wanasheria LEAT wanatoa wito kwa serikali -Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kuchukua hatua za dhati za kuanzisha Baraza la Rufani la Mazingira, anasema Thomas.

“Ni imani yetu kuwa miaka 16 ya uwepo wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 bila ya uwepo wa chombo hicho cha rufani ni ukwamishaji wa jitihada za usimamizi bora wa mazingira. Ni matumaini yetu kuwa wakati tuliokuwa tukisubiri ni sasa na ndiyo muda wa utekelezaji,” anaongeza.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# KWA HERI MWAKA 2020

- Ulitesa elimu, corona ilizuia masomo
- Moto uliua 10, kuchoma shule 33



Shule kuteketezwa moto na wanafunzi kuumizwa ni mambo yaliyotikisa sekta ya elimu 2020. **PICHA: ITV**

MWAKA 2020 unafika ukingoni na kama ilivyo miaka mingine, unaanza na kumalizika ukiwa na matukio mengi yakiwamo ya kusikitisha na kuumiza mioyo na mengine ya kufurahisha.

Kwa hapa nchini, kuanzia Januari hadi leo Desemba 29, yapo matukio mengi ambayo yalitokea lakini mahsusi 2020 ni uwapo wa maradhi ya COVID-19 na athari zake kwa elimu.

Lakini pamoja na COVID-19, uhai wa watoto shuleni ulitishiwa na moto na mikasa iliyotikisa ni pamoja na kuungua shule kadhaa na kuua wanafunzi 10.

**KITISHO CHA MOTO**

2020 ni mwaka ulioshuhudia moto ukizuka sehemu nyingi, lakini vifo viliripotiwa katika Shule ya Kiislamu ya Binamungu iliyoko Bukoba.

Katika ajali hiyo iliyotokea miezi mitatu iliyopita huko mkoani Kagera, wanafunzi 10 walipoteza maisha.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari mikasa hiyo ilianza Januari kisha kupungua, lakini baadaye ikaibuka tena kwa kasi kubwa baada ya wanafunzi kurejea shuleni kuanzia Julai.

Hali hiyo ilisababisha taharuki kwa wanafunzi hao kutokana na matukio ya vifo na uharibifu wa mali zao uliotokana na kuungua kwa majengo yakiwamo mabweni na hivyo walisoma kwa woga.

Baada ya wanafunzi kurudi shuleni kuendelea na masomo, matukio ya kuungua kwa majengo ya shule nayo yaliibuka upya, ambayo Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas (CP), anasema, ni miongoni mwa yalioshika nafasi kubwa mwaka huu.

Matukio hayo likiwamo kuchoma moto mabweni ya shule za sekondari za Uchira na Ebeneza Sango, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro ni miongoni mwa mambo yaliyotikisa mwaka.

Moto huo ulisababisha watuhumiwa watatu wakiwamo wanafunzi wawili na mwalimu wao kunaswa.

Kwa upande wake Sabas katika taarifa yake kuhusu matukio ya kuungua moto kwa majengo ya shule, anasema, kuna sababu tofauti, zikiwamo hitilafu za umeme, migogoro shuleni na uzembe, huku shule za watu binafsi na taasisi za kidini zilizoungua zikiwa ni 20 na za serikali 11.

"Jumla ya shule zote zilizoungua kuanzia Januari hadi Novemba mwaka huu ni 33, lakini kuna tatizo la baadhi ya wanafunzi kuacha masomo na kujiunga na makundi ya kihalifu," anasema Kamishna Sabas.

Kufuatia kuwapo kwa matukio hayo, anawaomba wazazi na walezi kufuatilia nyendo za watoto wao, kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la watoto kuacha shule na kwenda kujiunga na makundi ya kihalifu.

"Miongoni mwa wahalifu hao ni wale waliokuwa Kibiti na baada ya kudhibitiwa na vyombo vya ulinzi na usalama, walikimbilia nchi jirani ya Msumbiji," anasema.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo anasema, hadi sasa wapo wanafunzi waliokuwa wameacha shule na kujiunga na vikundi vya kihalifu ambao wamekamatwa wakiwa wanavuka kuelekea Msumbiji na wengine tayari wameishafanikiwa kuvuka kuingia nchini humo.

**CORONA NA ELIMU**

Tukio la kuibuka corona sehemu mbalimbali duniani, hatimaye kutua nchini Machi mwaka huu, kulisababisha serikali kufunga taasisi za elimu kuepusha wanafunzi na maambukizo ya maradhi hayo.

Serikali ilianza kuzifunga taasisi zote hizo kwa siku 30 kuanzia Machi 17, 2020, na kusitisha mkusanyiko wa watu, katika maeneo mbalimbali, kwa lengo la kukabiliana na kusambaa kwa ugonjwa huo hatari, unaosambaa kwa hewa, kugusa virusi na kugusana kwa majimaji ya mwili kama makamasi, damu, haja ndogo na mate kutoka kwa aliyeathirika kuingia kwenye mtu mwingine.

Wakati mwaka ukiumizwa na sakata la corona, ambalo lilisababisha wanafunzi hasa wa shule za msingi kusoma kwa miezi sita mtawalia, hata likizo yao ya mwisho wa mwaka kupungua.

Shule nyingi zilikuwa zimefungwa ilipofika Desemba 18 mwaka huu na kutarajiwa kufunguliwa kuanzia Januari 10 mwakani.

Corona itakuwa imesababisha likizo ya mwisho wa mwaka kufupika kiasi licha ya kwamba ratiba itakaa sawa baadaye.

Awali baada ya kutangaza likizo ya corona, serikali ilitangaza kufunga shule kwa muda wa siku 30, ili baada ya hapo wanafunzi warudi shuleni kuendelea na masomo, lakini baadaye ikalazimika kuirefusha likizo hiyo ili kusubiri hali itulie.

Katika likizo hiyo ya siku 30, shule zilitarajiwa kufunguliwa katikati ya mwezi Aprili, lakini haikuwa hiyo, badala yake ziliendelea kufungwa hadi mwishoni mwa mwezi Juni.

Juhudi mbalimbali zilikuwa zikifanyika katika kupunguza athari zitokanazo na virusi vya corona, ikiwa ni pamoja na watu kuvaa barakoa, kupiga nyungu na kutokaribiana, huku magari wakizuiwa kujaza abiria kupita kiasi.

Wazazi na walezi nao walihimizwa kutowaruhusu watoto wao kuzurura au kusafiri kwenda mbali, badala yake wabaki nyumbani kuepuka kuambukizwa ugonjwa huo ambao ulilazimisha shule kufungwa.

Huku wakiwa nyumbani, serikali ilikuwa ikitafuta mbinu za kuhakikisha wanaendelea na masomo kama kawaida badala ya kukaa tu wakisubiri likizo ambayo ilikuwa haijulikani itaisha lini.

**KUSOMEA NYUMBANI**

Kutokana na wanafunzi kuendelea kuwa na likizo, serikali iliamua kuanzisha vipindi vya masomo kupitia redio na televisheni ikiwa ni kuitikia wito wa shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Lengo la shirika hilo lilikuwa ni wanafunzi waendelee kujifunza hata wakati wakiwa nyumbani kutokana na janga la ugonjwa huo.

Hivyo, wizara ilizindua rasmi urushaji wa vipindi vya masomo kupitia televisheni na radio.

Kwa Tanzania uzinduzi huo ulifanywa jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk. Leonard Akwilapo, ambapo, vipindi hivyo vya masomo mbalimbali kuanzia elimu ya awali hadi ngazi za juu viliidhinishwa rasmi kutangazwa.

Vipindi hivyo vilihusu pia wanafunzi wa shule za msingi na kidato cha kwanza mpaka cha sita, huku vikisambazwa katika vyombo mbalimbali vya habari nchini ili masomo yaweze kufikia wanafunzi wote nchi nzima kwa wakati.

Wizara ya Elimu iliandaa vipindi hivyo kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania, lengo kubwa likiwa ni kuwawezesha wanafunzi waendelee kujifunza wakati wote wa likizo hiyo iliyotokana na kuwaepusha wanafunzi na maambukizi ya corona.

Shule binafsi nazo hazikubaki nyuma kwa wanafunzi wake, kwa kuwa ziliandaa masomo na kutuma kwa wanafunzi kwa njia ya mtandao, huku wengine wakipelekewa nyumbani kwao au kusoma kwa njia ya kompyuta au mikutano ya kimtandao ya 'zoom'.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# KERO ZILIZOUDHI WENGI ZINABEBWA KUINGIA 2021

ZIMETIMIA siku 365 tangu kuanza mwaka huu ambao keshokutwa unamalizika, hivyo kuanza kufungua kalenda mpya ya 2021.

Inawezekana 2020 umekuwa ukumbusho kimaisha kwa wengine au machungu na huzuni zisizosahaulika kwa baadhi. Yaliyopita si ndwele karibu 2021, lakini unapoingia ni wakati wa kutazama nyuma kuangalia yale yaliyowakera wengi mijini na vijijini.

Yaliyowafurahisha ni mengi, lakini zipo kero zinazovuka mwaka na kuendelea kutesa kwa vile hazijapata ufumbuzi, pengine zitavuka mwaka? Mojawapo ni hizi.

USAFIRI UNAOCHOSHA

Usafiri wa kubanana ndani ya magari hasa mijini ni changamoto inayozidi kukua hasa kwenye majiji na miji mikubwa. Wengi walidhani kuwa ujio wa mabasi ya mwendokasi ungepunguza tatizo hilo Dar es Salaam, lakini shida imeongezeka zaidi.

Watu wanabanana na kusongana kupindukia ndani ya magari hayo tatizo ambalo linaendelea hata Ijumaa unapoanza mwaka mpya kubanana kuko pale pale iwe kwenye mabasi ya mwendokasi 'express' na daladala nyingi mijini.

**BIDHAA BARABARANI**

Mambo haya ya kukuta barabara na sehemu wanaokwenda kwa miguu zimejaa bidhaa. Kila kitu kimepangwa chini kuanzia vyakula -matunda, mavazi na mboga.

Wapo samaki wabichi na wakukaanga, chips, ndizi, mahindi ya kuchoma na kuchemsha na bidhaa za urembo.

Ni kero zinazoshuhudiwa kwenye vituo vingi vya mabasi Dar es Salaam sehemu za Mbezi, Kimara, Mbagala, Ilala na Buguruni.

Hali ni vivyo hivyo Mbeya kama Mwanyelwa na Dodoma, makao makuu ya nchi, hata Mwanza mtaa wa Makoroboi.

Ni shida inayoonekana pia kwenye vituo vya mabasi ambavyo ukweli ni kwamba hakuna sehemu isiyo na bidhaa labda chini ya gari.

KUSUBIRI HOSPITALINI

Mwaka unapoanza kuna baadhi ya watu ni wagonjwa. Wapo waliowahi saa 10 alfajiri kusaka namba ya kumuona bingwa. Unafika saa 11:30 alfajiri unapata namba 70 na unaweza kukaa hospitalini hadi saa 10 jioni.

Ni changamoto ambayo inahitaji ufumbuzi kwa vile kuanza kusaka huduma saa 11 alfajiri hadi saa 10 jioni ni usumbufu, yataka moyo.

**WANAFUNZI VITUONI**

Ni miongo mingi wanafunzi wanaendelea kusota vituoni wakisubiri usafiri. Kwa Dar es Salaam kila mwaka hali ikiendelea kuwa mbaya. Ni wa shule za msingi hadi za sekondari za serikali wanaomaliza masomo jioni ni



Biashara barabarani kwenye miji na majiji ni kero kwa wasafiri, wakazi na hata vyombo vya usafiri. **PICHA: MTANDAO**

waathirika wakubwa.

Vituo vingi vya daladala bila kujali ni kikubwa au kidogo kina wanafunzi wengi kuanzia saa 10 hadi saa 2:00 usiku.

Imekuwa ni mazoea makondakta kuwakataa wanafunzi hao na hata kuwasukuma wasipande magari yao. Vitimbi vya kuwakataa vinaanza kwa kuwalazimisha kulipa nauli ya abiria watu wazima. Vingine ni kuwazuia milangoni na kupambana nao. Vitisho kama gari hili siyo darasa, wako wenzenu kibao subirini jingine ni mambo yanayoshuhudiwa.

Abiria hawajaweza kuwatetea wanafunzi. Wazazi hawajafikiria kuwakodia watoto wao usafiri, yote hayo yameongeza shida kwa watoto hao wanaoamka saa 10 alfajiri na kurudi nyumbani saa 4:00 ni suala la kutafakari mwaka 2021. Wazazi, walezi na wadau jiongezeni.

**MAKONDA BADO WACHAFU**

Makondakta wa daladala mna shida gani? Ni watu ambao mavazi yao kwa miaka mingi ni 'balaa'. Wanavaa suruali tatu, lakini zote hazina zipu. Zinafungwa na kamba za mkonge. Mashati yamepauka, kuchakaa na hayana vifungo.

Mwaka unapoanza watoa huduma hawa wajitafakari kwanini hawana unadhifu? Hawana jukumu jingine la kuwapatia kipato mbali na kazi ya kuhudumia abiria kwanini wasiwe na unadhifu?

Kama madereva wa mwendokasi ni watanashati wa daladala nao kwanini wasilazimishwe? Ni kero kwa abiria wanaoteseka na harufu mbaya za vinywa, viatu na mavazi. Jirekebisheni inapoanza 2021. Vyama vya wasafirishaji na watoa huduma rekebisheni kero hii iliyopevuka.

**BODABODA HIZI**

Sekta ya usafiri zama hizi iko mikononi mwa pikipiki, lakini nazo kama daladala madereva wake ni kero. Wanavaa nguo chafu, wengi wana harufu mbaya za vinywa, miili , wengine hawana viatu na kwa ujumla ni sekta muhimu lakini wahudumu wake hawajajitambua.

Kama ilivyo kwa daladala hata waendesha bodaboda nao wana vyama wawe na kanuni na sheria zao vijiweni zinazolazimisha usafi na kuzingatia yampasayo mtoa huduma za umma.

**WAPIGADEBE HADI LINI?**

Ni kero kila kituo cha mabasi kiwe kikubwa kidogo au cha mabasi ya mikoani wapiga debe ni kero. Watu wamechoka. Daladala zimechorwa mistari na kupakwa rangi za utambulisho wa ruti zake, lakini bado.

Si hivyo tu, zimeandikwa zinapoelekea, lakini kelele za wapigadebe hazikomi. Tunaiuliza Mamlaka ya Usafirishaji Nchi Kavu (LATRA) pamoja na Kikosi cha Usalama Barabarani kupigadebe vituoni ni sehemu ya ajira rasmi? Kama sivyo wanafanyanini hadi leo 2021? Hamjasikia kuwa wengi wao ni wadokozi wanaoibia abiria? Wasaidieni wasafiri wawe na amani.

**KUWATUSI WANAWAKE**

Mazoea ya matusi ya nguoni yanayotaja viungo vya siri vya wanawake yanaanza kukubalika na inakuwa ni kawaida kusikia wakitukanwa muda wote iwe kwenye vyombo vya usafiri, mikusanyiko, barabarani na popote wanaume wanapotofautiana.

Inavyoelekea linakuwa jambo linalowapendeza wengi kwa vile halikemewi wala hakuna anayeona kuwa ni mmomonyoko wa maadili. Inawezekana kuwa hivyo kwa sababu viongozi wa ngazi mbalimbali wanasikia matusi hayo pengine wakiwamo polisi, wabunge hata wanasheria na mawakili wa serikali lakini haijasikika mtuhumiwa kushtakiwa kwa kutukana matusi ya nguoni hadharani.

**KUVUTA HADHARANI**

Kuna usemi kuwa wanaovuta sigara 'wanawaua' wasiovuta. Hicho ndicho kinachotokea kwenye vituo vya mabasi, sokoni, barabarani bila kujali ni vijijini au mijini. Watu wanavuta ovyo na kuwapumulia moshi wengine.

Wapo wanaovuta hata karibu na watoto wadogo. Hili nalo litaendelea hadi lini? Mwaka 2021 uje na mabadiliko maana watu wanachoka kupumuliwa moshi na 'mateja wa fegi', kama kuna sheria itangazwe na mabango yabandikwe sehemu za umma kuondoa mazoea ya kuendelea kuvuta sigara kila mahali.

**KARAKANA ZA VYUMA**

Mitaani kuna karakana za kuchomelea vyuma zinazotengeneza madirisha, mageti na magari. Kinachotumiwa ni gesi hatarishi ambayo ni rahisi kulipuka na kusababisha vifo, kujeruhi na hata kulipua makazi.

Pamoja na kulipua makazi kuna uwezekano wa kuchangia watu kupofuka macho kutokana na mwanga mkali unaotokea wakati wa kuchomelea na kuunga vyuma.

Chonde chonde shida hii mpaka lini kwenye makazi ya watu? Serikali isisubiri mpaka yakatokea ya matangi ya petroli kulipuka na kuangamiza mamilioni. Kuja haja kwa mwaka 2021 kutafuta ufumbuzi kamili wa suala hilo.

**'SHELI' NA ABIRIA**

Kuna mazoea kuwa kila kituo cha mafuta huitwa sheli, licha ya kwamba kampuni ya Shell iliyokuwa inauza mafuta ilishafungwa na kuondoka nchini, hata hivyo kikubwa hapa ni maezoea na kero ya mabasi ya abiria kuendelea kuingia ndani ya vituo vya mabasi na abiria.

Yaliwahi kutolewa maelekezo, serikali ikipiga marufuku mabasi ya abiria kujaza mafuta wakati yakiwa na watu ndani, lakini jambo hilo linaendelea kupuuzwa. Mwaka unapoanza ni vyema kukumbusha kabla basi halijalipuka na kusababisha maafa.



# Kabaka aahidi makubwa UWT

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Taifa (UWT), Gaudensia Kabaka, ametangaza nia ya kuuwezesha umoja huo kujitegemea kiuchumi na kuachana na mazoea ya kuombaomba.

Aidha, amesema kazi yake kubwa ni kuhakikisha anawaongoza wanawake kufikia mafanikio kiuchumi ndani ya jumuiya hiyo, ili wajitegemee na kuepuka kuwa ombaomba wa fedha zikiwamo za uchaguzi kwenye ngazi zote.

Kabaka, aliyasema hayo wakati akizindua shule ya awali ya UWT kama moja ya kitega uchumi chao.

**Nimefurahi kuona Dodoma wameniita kuzindua vitega uchumi vyetu, nimetekeleza haraka kwa sababu ni moja ya maendeleo ya UWT.**

"Nimefurahi kuona Dodoma wameniita kuzindua vitega uchumi vyetu, nimetekeleza haraka kwa sababu ni moja ya maendeleo ya UWT," alisema Kabaka.

Aidha, akizungumzia uchaguzi, alisema hakuna anayebisha uchaguzi mkuu 2020 kinamama walijitoa kwa wingi kuhakikisha CCM inapata ushindi.

Alifafanua kuwa ametembelea mikoa mingi hapa na kushuhudia wanawake walivyokuwa wakijitoa kwenye mikutano ya hadhara ya ndani na hata ya kitaifa wakihudhuria kwa wingi na inaonyesha jinsi gani wanapenda maendeleo.

Alisema, siasa ni uchumi kwani hata katika kipindi cha uchaguzi zinahitajika fedha kwa ajili ya kuufanikisha hivyo ni lazima kuwa na vitega uchumi vya UWT na si kuwa ombaomba, ndio maana wanafanya bidii kuzindua miradi mikubwa.

Mwenyekiti wa UWT alisema, elimu ndiyo kila kitu muhimu katika maisha hivyo mradi huu wa shule ni mahsusi kwa jamii hivyo ni lazima watu wasome.

"Hakikisheni mnakuwa karibu na ofisi za elimu ili kupata maelekezo ya uendeshaji na kupata walimu bora," alisema Kabaka.

"Kuna wadhibiti ubora ili wasije kuifungia shule yetu kwa kukosea masharti inawezekana mmefanya mengi, lakini ili kufanikiwa lazima tuwe karibu na hao kutuoa maelekezo," alisema Kabaka.

Kaimu Katibu UWT, Mkoa wa Dodoma Secilia Ndalu, akitoa nasaha zake, alisema ni jambo la kihistoria kwa wanawake wa mkoa wa Dodoma kutengeneza vitega uchumi vyao.

Alisema walianza ujenzi Agosti 2018 hadi Desemba 2019 kwa kusafisha eneo la ujenzi ikiwamo pia kuwachangisha wadau mbalimbali kuwaunga mkono.

## TPSF Dodoma yataka maeneo ya uwekezaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Sekta Binafsi (TPSF), Mkoa wa Dodoma imeushauri uongozi wa mkoa, kuainisha maeneo ya kuwekeza ili kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa jana na mwakilishi wa TPSF Dodoma, Ringo Ilingo, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu fursa zilizopo mkoani hapa kwa jili ya miradi mbalimbali ya uwekezaji.

Alisema, baada ya Rais John Magufuli, kukihamishia kituo cha uwekezaji TIC, katika ofisi yake, ni imani yao kuwa itasaidia kuondoa urasimu uliokuwapo hivyo ni wakati sasa mkoa wa Dodoma kujipanga na kubainisha maeneo ya kuweka vitega uchumi mbalimbali.

Vile vile, alisema mkoa huo una maeneo makubwa kwa ajili ya uwekezaji ambayo yanatakiwa kuainishwa ili iwe rahisi kwa wawekezaji kuyatambua wakati wanapo yahitaji.

"Sasa ni wakati wa mkoa kuyabainisha maeneo kwa ajili ya uwekezaji, ili wanaotaka kuanza miradi yao wayatambue, kuyafikia na kuanza kuwekeza," alisema Ilingo.

Pia, alisema kuwa pamoja na uwepo wa maeneo hayo kwa ajili ya uwekezaji, mkoa huo unatakiwa kufanyia kazi upungufu na kasoro zilizopo.

Alisema kuwa moja kati ya upungufu huo ni maeneo mengi kutokuwa na miundombinu rafiki kwa ajili ya uwekezaji kama vile umeme na maji.

Aidha, alisema wawekezaji wa nje na ndani ya nchi wanatakiwa kuchagamkia kufanya uwekezaji katika Jiji la Dodoma, kutokana na eneo hilo kuonekana kuwa ndani ya miaka mitano ijayo litakuwa la kibiashara kuliko hata Dar es Saalam.

"Uzuri wa Dodoma ni jiji ambalo ukiwekeza bidhaa zako zinaweza kuyafikia masoko yote kwa sababu mkoa huu unaunganisha maeneo mengi iwe ndani na hata nje ya nchi, mfano kuyafikia masoko ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) pamoja na soko la COMESA," alieleza Ilingo.



Meneja Uhusiano Idara ya Kilimo na Biashara wa Benki ya NMB, Kanda ya Kati, Renatus Kamugisha (kulia), akizungumza na wakulima wa Kijiji cha Ndulugumi, Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma, mwisho wa wiki, kuhusu mikopo ya kilimo inayotolewa na NMB. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Chuo chasajili wapya 9,000

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Dodoma (UDOM) kimesajili wanfunzi 9,000 katika 11,000 waliodahiliwa kwenye shahada mbalimbali za awali.

Aidha, kati ya hao chuo kimedahili wanafunzi 600 wa shahada za juu na wanafunzi 101 wa shahada za uzamivu.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha UDOM, Profesa Fautine Bee, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari chuoni hapo.

Prof. Bee alisema UDOM imedahili wanafunzi 11,000 mwaka huu wanaosoma shahada za awali na mpaka sasa waliojisajili ni wanafunzi ni 9,000.

Alibanisha kuwa ushindani ulikuwa mkubwa na chuo kililazimika kuchukua wanafunzi wenye ufaulu wa juu ili kupata wanafunzi bora zaidi.

Alisema, katika ushindani huo wapo wanafunzi waliofaulu kwa kupata daraja la pili, lakini hawakuchaguliwa kuingia baadhi ya fani kama ya udaktari na sheria.

Aliongeza kuwa kutokana na ufaulu huo kukosa nafasi katika masomo hayo waliwashauri wahusika kuomba fani nyingine, ili kupata nafasi ya kujiunga na chuo hicho.

Pia, alisema katika mchakato wa udahili wa wanafunzi mwaka huu uongozi wa chuo umebaini kuwa chapa (brand) ya chuo hicho imeongezeka kutokana na kupokea maombi mengi ya wanafunzi kutaka kujiunga.

Kadhalika, alisema asilimia zaidi ya 40, ya wanafunzi waliomba kujiunga na UDOM kwenye msimu mpya wa masomo, hicho ni kiwango kikubwa ikilinganishwa na uwepo wa vyuo vikuu vingi nchini na vingine ni vikongwe.

Alisema chuo kimeendelea kuboresha mafunzo pamoja na kuhusisha programu za mafunzo kwa vitendo ili kuwajengea wahitimu uelewa mpana wa yale wanayojifunza.

"Nitoe mifano michache, wanafunzi wetu wa sanaa ya ngoma, uchoraji, ubunifu wa mavazi, ubunifu wa kielektroniki wamekuwa wakipata kazi mbalimbali wangali chuoni ambazo wanaweza kuzifanya na kuwaingizia kipato," alieleza.



# Mgawo wa maji waendelea kuwatesa wakazi Swaya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TATIZO la mgawo wa maji katika Kata ya Swaya, Halmashauri ya Mbeya, limeendelea kuwatesa wakazi wa eneo hilo, huku baadhi ya vijiji vikiwa havijafikiwa na huduma hiyo.

Wakizungumza wakati wa ziara ya Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, wananchi hao walidai kuwa maeneo yao yana vyanzo vingi, lakini hawapati huduma ya maji ya bomba licha ya kuwapo kwa mradi mkubwa.

Mmoja wa wananchi hao, Fadhili Mzee, alisema kwenye kata hiyo kuna mradi wa Swaya- Lupeta, ambao ulifanyiwa usanifu miaka 10 iliyopita, lakini utekelezaji wake unasuasua bila sababu ya msingi.

Alisema mradi huo ulifanyiwa usanifu kulingana na idadi ya watu wakati huo katika vijiji, lakini utekelezaji ambao unafanyika sasa hivi umezingatia idadi ile ile ya zamani hali inayosababisha maji hayo kutokidhi mahitaji.

Alisema kwa sasa wananchi hao wanalazimika kuyapata kwa mgawo, huku baadhi ya vijiji vikikosa huduma hiyo kutokana na mradi huo kutokamilika.

**Baadhi ya watendaji hao walishafukuzwa kazi na wengine walifikishwa mahakamani kutokana na ufisadi walioufanya kwenye miradi hiyo.**

"Hatuelewi huyu mkandarasi ilikuwaje mpaka akaacha mradi huu, lakini hata ungekamilika bado haukidhi mahitaji ya watu tuliopo hapa kwa sasa, kwa hiyo hii shida ya maji ni kubwa tunaomba mbunge utusaidie kuitatua," alisema Mzee.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Lupeta katika kata hiyo, Edward Mwakijale, alisema kuna baadhi ya vitongoji katika kijiji hicho havipati huduma hiyo na hivyo wananchi kulazimika kutembea umbali mrefu kuitafuta.

Alivijata vitongoji hivyo kuwa ni Ibanga na Papyo pamoja na vijiji jirani vya Wimba na Nsenga na kwamba endapo utekelezaji wa mradi huo ungezingatia idadi ya wananchi kusingekuwapo na tatizo hilo la uhaba wa maji.

Aliiomba serikali kuwasaidia kuukamilisha mradi huo wa Swaya-Lupeta ili vijiji na vitongoji vyote vinufaike na pia unatakiwa utekelezwe kulingana na idadi ya watu waliopo kwa sasa, huku akidai kuwa ikiwezekana usanifu ufanyike upya.

Akizungumzia kero hiyo, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alikiri kutambua miradi hiyo ambayo haijakamilika kwa muda mrefu na kutaja sababu kubwa ya miradi hiyo kushindwa kukamilika kuwa ni baadhi ya watendaji wa serikali kutafuna fedha zilizokuwa zimetengwa.

Alisema baadhi ya watendaji hao walishafukuzwa kazi na wengine walifikishwa mahakamani kutokana na ufisadi walioufanya kwenye miradi hiyo.

Alisema awali walikuwa wanawatuhumu zaidi makandarasi waliokuwa wanatekeleza miradi hiyo, lakini baadaye wakaamua kuwa wawazi kwa kuwafichua watendaji waliokuwa wametafuna fedha hizo.

"Makandarasi walisema kabisa kwenye mikutano kwamba wao huwa wanalaumiwa mara nyingi, waliamua kusema kwamba waliotafuna fedha ni wanaokaa 'high table' (Meza Kuu) wakiwamo wakurugenzi," alisema Njeza.

Alisema katika harakati za kufuatilia miradi hiyo alipata matatizo ambayo hakutaka kuyaweka wazi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akimsikiliza mmoja wa wasimamizi wa maghala ya kuhifadhia mbolea, Iyunga jijini Mbeya, wakati akikagua hali ya upatikanaji wa mbolea jijini humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Taasisi ya Tulia yatoa msaada saruji mifuko 100

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, kupitia Taasisi yake ya Tulia Trust, ametoa msaada wa mifuko 100 ya saruji katika Shule ya Sekondari Lupeta iliyopo Kata ya Iyunga jijini hapa, kwa ajili ya ukarabati wa vyumba vya madarasa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Dk. Tulia aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na kujitolea katika kutatua matatizo yanayozikabili shule mbalimbali kwenye maeneo yao, kwa kuwa shule hizo ni mali yao.

Alisema aliamua kuchangia mifuko hiyo ya saruji baada ya kupata taarifa ya uwapo wa baadhi ya matatizo kwenye shule hiyo na kuamua kuungana na wananchi wake kutatua akianzia na ukarabati wa majengo.

Alisema vyumba hivyo vinatakiwa vikarabatiwe haraka, ili wanafunzi wote wa kidato cha kwanza waliochaguliwa kujiunga na shule hiyo waanze mapema masomo na wasitofautiane na wenzao.

"Kila mzazi anatamani mtoto wake apate elimu bora na afaulu vizuri, lakini vyote hivyo vinafanikiwa katika mazingira yaliyo bora, sasa ni lazima tushirikiane katika kuboresha mazingira ya shule zetu," alisema Dk. Tulia.

Alisema elimu ni muhimu kwa ajili ya kuandaa viongozi bora wa baadaye na kuwataka wazazi na walezi wa watoto waliofaulu kuhakikisha watoto wao wanaenda shuleni kama ilivyokusudi la serikali.

Alisema kwa sasa hakuna kisingizio chochote cha mtoto kutoenda shuleni kwa kuwa serikali inagharamia elimu na kazi ya mzazi ni kuhakikisha mtoto anapata vifaa na sare za shule pekee.

# Viwanda vya mafuta vyafungwa kisa uhaba malighafi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wamiliki wa viwanda vya kuzalisha mafuta ya alizeti jijini hapa wamelazimika kufunga shughuli zao kutokana na kukosa malighafi, huku bei ya mafuta hayo ikipaa kipindi cha msimu wa sikukuu.

Kupaa kwa bei ya mafuta ya kupikia kunadaiwa kuathiri shughuli zingine za kiuchumi ikiwamo biashara za vyakula.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wamiliki wa viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti vilivyopo katika Soko la Sido jijini hapa, walisema mwaka huu umekuwa tofauti na miaka mingine kutokana na malighafi kuisha mapema zaidi.

Mmoja wa wamiliki hao, Charles Mwakitalima, alisema uhaba wa malighafi hiyo umetokana na mvua zilizonyesha kupita kiasi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambazo ziliharibu alizeti mashambani.

Alisema wakulima walijitahidi kulima kwa wingi zao hilo, lakini baada ya mvua kuzidi ziliharibu na kusababisha kuoza zikiwa bado ndogo shambani, huku baadhi zikioza baada ya kukomaa wakati mvua ikiendelea kunyesha.

"Miaka iliyopita, miezi kama hii tunakuwa bado tuna malighafi za kutosha na hata bei ya mafuta ilikuwa haipandi kama ilivyojitokeza mwaka huu, na hii huwezi ukamlaumu mtu kwa sababu ni matatizo ya hali ya hewa ambayo hayasababishwi na mtu," alisema Mwakitalima.

Naye Samson Sangwe, ambaye ni mmoja wa wafanyakazi kwenye moja ya viwanda hivyo, alisema kwa sasa hakuna biashara ya mafuta wala mashudu kutokana na kukosekana kwa malighafi.

Alisema wamiliki wa mashine hizo wanalazimika kuzifunga kwa sababu gharama za uendeshaji ni kubwa kuliko wanachopata, akaiomba serikali kukabiliana na tatizo hilo la uhaba wa mafuta.

Baadhi ya wafanyabiashara wa chakula maarufu mamalishe na baba lishe, walisema kuadimika kwa mafuta na kupanda bei kumesababisha biashara zao kukwama kutokana na wengi wao kushindwa kumudu bei.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Debora Mwanyanje, alisema mafuta ambayo awali walikuwa wananunua Sh. 15,000 lita tano, kwa sasa wananunua Sh. 25,000 bei ambayo alidai ni kubwa kuwahi kutokea tangu alipoanza kufanya biashara hiyo.

Alisema: "Chips kavu bado tunauza Sh. 1,000 na maandazi Sh. 200, sasa wengine wameshindwa kuendelea na biashara na nina wasiwasi hata sisi tutashindwa kuendelea kwa sababu ukipiga hesabu unajikuta kila siku unaingia hasara au unapata faida kidogo," alisema Debora.



# Mkuu wa wilaya atishia kuufungia mgahawa chuo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kati, Hamida Mussa Khamis, amemwagiza Mkurugenzi wa Baraza la Mji Kati kuufungia mgahawa wa Chuo Kikuu cha Zanzibar kutokana na kukiuka taratibu za uendeshaji.

Akizungumza jana baada ya kutembelea chuo hicho huko Kibele Wilaya ya Kati Unguja, alisema haridhishwi na hali ya mazingira ya mgahawa huo pamoja na wanaotoa huduma kukiuka taratibu za uendeshaji ikiwamo kupima afya na kupatiwa vyeti na kutokuwa na leseni ya biashara hiyo.

Alisema kuendelea kuuacha mgahawa huo kutoa huduma kwa wanafunzi na walimu wa chuo hicho, kutasababisha matatizo ya kiafa kwa wanafunzi.

Alisema serikali ya wilaya, imeona umuhimu wa kuufunga kutoa huduma ya vyakula hadi watakapotimiza taratibu za uendeshaji.

Vile vile, aliuagiza uongozi wa chuo hicho kufanya matengenezo ya haraka vyoo vya bweni vya wanafunzi wa kike kutokana na mazingira ya vyoo hivyo kuwa vichafu.

Alisema endapo kitashindwa kutekeleza agizo hilo, serikali ya mkoa itafunga huduma za bweni.

Kwa upande wake Mkuu wa Utawala wa chuo hicho, Profesa Mohamed Makame, alisema watavifavyia matengenezo kwa haraka vyoo hivyo, ili wanafunzi wanaopata huduma ya bweni kuwa katika mazingira salama.

**Endapo kitashindwa kutekeleza agizo hilo, serikali ya mkoa itafunga huduma za bweni.**

# Apongeza kasi ya viongozi kukabili kero za wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Hemed Suleiman Abdulla, amepongeza kasi kubwa ya viongozi wa majimbo katika mwelekeo wao wa kuondoa kero zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

Hemed alitoa pongezi hizo juzi, wakati akizungumza na wana-CCM na wananchi wa Jimbo la Chumbuni, katika mkutano wa hadhara wa kutoa shukrani baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. Mkutano huo umekwenda sambamba na mwanzo wa utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi ndani ya Jimbo la Chumbuni pamoja na utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na viongozi wa jimbo hilo wakati wa kampeni za uchaguzi.

Alisema hilo ni jukumu kubwa lililobebwa na viongozi hao likilenga kwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025.

**Zipo changamoto zilizokuwa zikikwaza utendaji wa serikali ikiwamo kero ya rushwa, uzembe na ubadhirifu aliokusudia Rais kuuondoa.**

Hemed ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, aliwaomba viongozi wa majimbo mengine kuiga mfano wa viongozi wa Jimbo la Chumbuni lililoanza safari ya utekelezaji huo uliyoonyesha mwanzo mwema wa mafanikio katika ustawi wa kijamii.

Aliwataka wananchi watakaobahatika kupata nyenzo za kuendeleza miradi ya ujasiriamali kuhakikisha vyerehani walivyokabidhiwa vinaendelea kuwahudumia na kuonya kwamba haitapendeza kutokea siku zana hizo zikakutwa sokoni.

Hemed aliwahakikishia viongozi na wananchi wa Jimbo la Chumbuni kuwa serikali iko tayari kuzipokea changamoto za wananchi hao ambazo haziko kwenye uwezo wao wa kuzitatua.

Akizungumzia suala ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Zanzibar, aliwataka wananchi kumvumilia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiendelea kupanga safu ya uongozi.

"Zipo changamoto zilizokuwa zikikwaza utendaji wa serikali ikiwamo kero ya rushwa, uzembe na ubadhirifu aliokusudia Rais kuuondoa," alisema.

Akielezea mikakati ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, Mwakilishi wa jimbo hilo, Miraji Khamis Mussa, alisema zipo changamoto kadhaa zitakazoshughulikiwa na uongozi katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa zinazohitaji nguvu, waliomba serikali iwaongezee nguvu akitolea mfano mtaro wa maji machafu ambao msimu wa mvua kubwa za masika huleta athari zinazosababisha baadhi ya wananchi wa eneo husika kuhama.

Naye Mbunge wa jimbo hilo, Ussi Salum Pondeza, alisema mabalozi wa CCM ndani ya jimbo hilo wamefanya kazi kubwa ya kukipigania chama hicho na matokeo yake wananchi walio wengi wameamua kuipa ridhaa CCM kuendelea kuongoza dola.

Alisema mwanzo wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 hadi 2025 kasi yao inaanzia katika kuwapa nguvu mabalozi katika ile dhana nzima ya kuthamini uzalendo wao na hatimaye CCM inazidi kunawiri.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akimkabidhi mmoja wa mabalozi wa Jimbo la Chumbuni, vyerehani 120 kati ya 160 vilivyotolewa na uongozi wa jimbo hilo, kutekeleza ahadi aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi. **PICHA: OMPR**

# Mwinyi kuunda tume uchunguzi kuporomoka jengo la ajabu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema atatunda tume kuchunguza sababu ya kuporomoka jengo la maajabu (Bait-El-Ajab), ambalo ndio sura na kivutio cha Zanzibar.

Akizungumza jana na wananchi wanaoishi katika Mji Mkongwe, alisema tume hiyo itasaidia kujua sababu ya kuporomoka kwa jengo hilo ambalo ni urithi wa dunia.

"Jengo la Bait-El-Ajab ndio sura ya Zanzibar hivyo hatupo tayari kuona sura hiyo inatoweka hivyo ni vyema kufanya juhudi za haraka kulirejesha jengo hilo katika hadhi yake," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema tume hiyo pia itatoa ushauri wa nini kifanyike ili Mji Mkongwe uendelee kuwa katika urithi wa dunia.

Vile vile, aliagiza kufanyike matengenezo ya majengo yote mabovu katika Mji Mkongwe ili kuepusha maafa mengine.

Awali, katika kikao hicho, wananchi wanaoishi katika eneo hilo walisema kuwa urasimu uliopo katika Mamlaka ya Mji Mkongwe unasababisha kuporomoka kwa majengo ya mji huo.

Baraka Shamte, mkazi wa Mkunazini, alisema katika Mamlaka ya Mji Mkongwe kuna urasimu mkubwa wa kutoa vibali vya kufanya matengenezo majengo hayo.

"Mheshimiwa Rais Majengo mengi ya Mji Mkongwe yapo katika hali mbaya, lakini tunapoomba kibali kwa ajili ya kufanya matengenezo tunanyimwa," alisema Shamte.

Jengo la Bait-El- Ajab liliporomoka Desemba 25 na kusababisha maafa ya watu wawili kufariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa.

Waliofariki katika tukio hilo ni Pande Makame Haji (25), mkazi wa Bububu na Burhan Ali Makuno (35), mkazi wa Mtoni Kidatu.

Waliojeruhiwa ni Ali Ramadhan (28), mkazi wa Kinuni, Haji Juma Machano (24), mkazi wa Chumbuni, Hamad Mattar (35) na Zamir Salum (40), wakazi wa Kinuni ambao wote walikuwa wakiendelea na shughuli za ujenzi katika jengo hilo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

**OFISI ZA MATANGAZO**

Mikocheni Industial Area,

Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.

E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

## CHETI KIMEPOTEA



**BAHATI WILLIAM KAMANDO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **No.S1791-0083** kilichotolewa na Baraza la mtihani kupitia **MVUMI MAKULU SECONDARY SCHOOL** mwaka **2009.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/873320/2020.**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA**
**MAHALI MASWA**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 146 YA MWAKA 2020**
**KATI YA**
**NKOBA WINOGELA............ ..................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1.CHARLES BUSHUNGU**
**2.JIYOJA ZENGO..................................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/ TAARIFA**

Kwa; **CHARLES BUSHUNGU NA JIYOJA ZENGO POPOTE MLIPO KATIKA JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi dhidi yenu, katika Baraza hili la wilaya ya Maswa, Maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani, mnatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wenu wa maandishi(WSD)kabla ya **tarehe 14.01.2021.**

Pia mnajulishwa kuwa maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya **tarehe 14.01.2021** saa **2;30** asubuhi mbele ya Mhe J.F.Kanyerinyeri Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na nyumba wilaya- Maswa.

Napia mnafahamishwa kuwa iwapo mtakaidi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yenu.

**IMETOLEWA kwa MKONO** wangu na **MHURI** wa Baraza hili tarehe **10.12.2020.**

**J.F KANYERINYERI**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MASWA.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MOSES S. MBILINYI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD** aina ya **FEKON** namba za usajili MC 530 Chassis No. LDAPAJOB2KGB07006,Engine **No. 157FM1219F07006.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DOM/RB/32011/2020.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No....OF 2020**

In the matter of the Estate of the late **REGINA RAPHAEL SILLO** of **Nzuguni** within Dodoma city

And

In the matter of Application for Probate by **ELIUD EDWARD MAHENGE**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 30 day of 12 ,2020.

**Dated at Dodoma this 16 December 2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KILOSA**
**S.L.P. 29, KILOSA**
**29-09-2020**

**YAH: MAOMBI MADOGO NA: 08/2020.**
**DICKSON MMARI.................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**KEDHIA L.MOROGORO.........WAJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA KEDHIA L.MOROGORO.**

Popote Ulipo unaarifiwa Ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Kilosa tarehe **14/01/2021.**Wenyewe binafsi au Mwakilishi wako bila kukosa ambapo **MAOMBI** yamepangwa kutajwa. Endapo hutaudhuria,maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imesainiwa leo **Tarehe 29 Mwezi 09** Mwaka **2020.**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**RUFAA YA SHAURI LA MADAI/TALAKA Na. 02 YA 2020 M/WILAYA NYAMAGANA (Imetokana Na Madai/Talaka Na. 95 Ya 2019 Katika M/Mwanzo Mjini) LETICIA CHRISTINE --------------------------------MDAI**
**DHIDI YA**
**GILBERT GOZBERT ---------------------------------MDAIWA**

**M/MWANZO YA ILEMELA - SHAURI LA MADAI Na. 106/2017**
**HAPPIFANIA LINUS.........................................................MDAI**
**DHIDI YA**
**ANDREA YAKOBO BULALO...................................MDAIWA**

**M/MWANZO YA MKUYUNI - SHAURI LA MADAI Na. 37/2020**
**REBECA AYUBU.................................................MDAI**
**DHIDI YA**
**PASCHALSILVESTER..........................................MDAIWA**

**M/MWANZO YA MJINI - SHAURI LA MADAI Na. 43/2020**
**YASINTA NELIWAKOLOSPERU................................MDAI**
**DHIDI YA**
**FELIX MWESIGA ...............................................MDAIWA**

**M/MWANZO YA MISUNGWI - SHAURI LA MADAI Na. 15/2019**
**PILI ATHUMAN MASAZA ............................ .......................MDAI**
**DHIDI YA**
**UNDI TANGA JILALA.............................................. MDAIWA**

**KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO YA MKUYUNI, MAHAKAMA YA ILEMELA, MAHAKAMA YA MWANZO MJINI NA MAHAKAMA YA MWANZO MISUNGWI, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WANANDOA AMBAZO NI NYUMBA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.**

| SN | MALI | MAHAL | MUD |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA | MTAA WA NYALUHAMA- | 28/1/2021 SAA 4 ASUBUHI NA |
| 2 | BOMA LA NYUMBA | MTAA WA KUZENZA-NYEGEZI | 29/1/2021 SAA 4 ASUBUHI NA |
| 3 | NYUMBA | MTAA WA MKUDI-GHANA NYUMBA | 1/2/2021 SAA 4 MCHANA NA KUENDELEA |
| 4 | NYUMBA | IGOMA BLOCK C NA 6 | 2/2/2021 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5 | NYUMBA | KIWANJA NA 39 KITALU "B" | 3/2/2020 SAA 4 ASUBUHI NA |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. **MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.**
2. **GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.**

**MAWASILIANO: 0768-588155/0782-405140**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Polisi yadaiwa kutumia nguvu dhidi ya upinzani

**Kampala, UGANDA**

MLINZI wa Bobi Wine 'Robert Kyagulanyi' inadaiwa ameuawa katika mazingira ya kutatanisha, mwishoni mwa wiki.

Ripoti za vyombo vya habari Uganda, vinakariri mashahidi wakisema kwamba Francis Kalibala, aligongwa na gari la Jeshi la Uganda UPDF, wakati msafara wa Bobi Wine ulikuwa unarudi Kampala kutoka Masaka katika kampeni.

Katika taarifa kupitia mitandao ya kijamii Bobi Wine alisema "nasikitika kutangaza kifo cha mmoja wa walinzi wangu Francis Kalibala, aliyegongwa na gari la jeshi namba H4DF 2382 ambalo liliziba njia karibu na Busega na kutuzuia kupita," aliandika Bobi Wine na kuongeza...

"Francis amefariki muda mfupi baada ya kufika katika Hospitali ya Rubaga."

Msemaji wa Jeshi la Uganda Brigedia Flavia Byekwaso alisema katika taarifa kwa vyombo vya habari kwamba, Francis, alianguka kutoka kwenye gari lililokuwa linaendeshwa kwa mwendo wa kasi.

"Francis hakugongwa na gari la jeshi. Alianguka kutoka kwenye gari namba UBF 850Z," alisema Byekwaso katika ujumbe wa twitter.

Kabla ya tukio hilo, waandishi kadhaa wa habari walishambuliwa na polisi na kujeruhiwa vibaya.

Waandishi hao walikuwa wanafuatilia tukio ambalo polisi walimzuia Bobi Wine, kufanya kampeni na kuzua makabiliano kati ya polisi na wafuasi wa Bobi Wine katika mji wa Masakaa.

Waandishi walipigwa na kujeruhiwa na mabomu ya kutoa machozi wengine walilazwa hospitali ya mjini Masaka.

Miongoni mwao ni mpigapicha wa televisheni ya Bobi Wine ya Ghetto TV, Ashraf Kasirye, mwandishi wa shirika la habari la Nation Media Group - NTV Ali Mivule.

"Gesi ya kutoa machozi ilitumika kutawanya wafuasi wa Bobi Wine na kwa bahati mbaya waandishi wa habari walijeruhiwa," alisema msemaji wa polisi, Fred Enanga.

Tume ya uchaguzi, imepiga marufuku kampeni katika wilaya na miji kadhaa ikisema kwamba wilaya hizo zina idadi kubwa ya maambukizi ya virusi vya corona na huenda kampeni zinaeneza virusi hivyo hatari.

Wilaya hizo ni pamoja na Mbarara, Kabarole, Luweero, Kasese, Masaka, Wakiso, Jinja, Kalungu, Kazo, Kampala na Tororo.

Wanasiasa wa upinzani hata hivyo wamesema hatua hiyo ni ya kisiasa kwa sababu sehemu ambapo kampeni zimepigwa marufuku ni ngome za kisiasa hasa za mgombea wa urais Bobi Wine.

Rais Yoweri Museveni, ambaye anagombea urais kwa muhula wa sita, amemaliza kufanya kampeni katika baadhi ya sehemu hizo na ndizo ambazo zimesalia kwa Bobi Wine.

Tume ya uchaguzi hata hivyo, ilisema kwamba Rais Museveni anaweza kuendelea kuzindua miradi ya serikali katika sehemu ambazo kampeni zimepigwa marufuku.

"Hatua ya tume ya uchaguzi imeniathiri sana. Wilaya ya Wakiso ina wapigakura milioni 1.5, Kampala ina wapigakura milioni moja, Jinja na Masaka zina maelfu ya wapigakura. Najiuliza, ni wapi nitatoa kura iwapo sitafanya kampeni?" Alisema Jenerali Henry Tukukunde, mgombea wa urais.

Wagombea wa viti mbalimbali wametakiwa kutumia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kufanya kampeni, huku idadi ya wapigakura katika wilaya ambako tume ya uchaguzi imepiga marufuku kampeni ya moja kwa moja ni Kampala 1,281.308, Wakiso 1,160,551, Kasese 372,102, Mukono 354,047, Jinja 274,772, Tororo 264,222) na Luweero 256,454

Kamanda wa kikosi maalum cha jeshi kinachomlinda Rais Museveni, Luteni Jenerali Muhoozi Kainerugaba, ameonya akiwataja kama wakoloni wanaounga mkono upinzani nchini Uganda, akisema kwamba watashindwa vibaya sana katika uchaguzi mkuu wa Jnauari 14.

Muhoozi aliandika kwenye twitter, baada ya wakili wa Bobi Wine Robert Amsterdam kuandika ujumbe wa twitter, akitaka jumuiya ya kimataifa kuingilia kati na kuwaajibisha maofisa katika serikali ya Uganda baada ya polisi kuwajeruhi waandishi wa habari Jumapili asubuhi.

Muhoozi alijibu ujumbe huo kwamba wakoloni wanajaribu kubadilisha rangi yao, lakini kila mzalendo anawajua.

***VOA***



Mwandishi wa habari, Zhang Zhan wa China, ambaye amepatikana na kosa la kuandika habari kuhusu mlipuko wa kwanza wa virusi vya corona katika mji wa Wuhan, amehukumiwa kifungo cha miaka minne jela.**PICHA/BBC**

# CAR yafanya uchaguzi licha ya vitisho vya waasi

**Bangui, CAR**

WANANCHI wa Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) wanaendelea kusubiri uamuzi wa Tume ya Uchaguzi, kuhusu uchaguzi uliofanyika Desemba 27, mwaka huu.

Licha ya baadhi ya vituo vya kupigia kura kutofunguliwa, huku baadhi ya wapigakura wakisalia nyumbani kwa hofu ya kuuawa katika maeneo yanayodhibitiwa na waasi.

Kulingana na vyanzo rasmi kutoka CAR, vituo 800 vya kupigia kura havikufunguliwa nchini kote kwa jumla ya vituo 5,400, sawa na asilimia 15.

Licha ya matatizo kadhaa yaliyojitokeza, uchaguzi ulifanyika kwa amani katika mji mkuu wa Jamhuri ya Afrika ya Kati, Bangui, na katika baadhi ya miji mikubwa.

Milio ya risasi ilisikika katika mji wa Bangui usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili, lakini hali ya usalama ilirudi kuwa shwari, baada ya vikosi vya usalama kupelekwa katika maeneo mbalimali ya mji huo, vikisaidiwa na walinda amani wa Umoja wa Mataifa na wanajeshi wa Rwanda.

Mgogoro huo ulisababisha wakazi wengi katika taifa hilo lenye utajiri wa almasi na dhahabu kushikwa na hofu ya kutumbukia tena katika machafuko kama yaliyotokea miaka ya nyuma. Uchaguzi wa CAR, ulitajwa kuwa mtihani muhimu kwa nchi hiyo yenye matatizo makubwa ya usalama.

Makundi ya wapiganaji yanadhibiti theluthi tatu ya CAR, ambayo sehemu kubwa ya watu ni maskini sana.

Serikali imekuwa ikimshutumu aliyekuwa rais wa nchi hiyo Francois Bozize kwa kupanga kupindua utawala wa Faustin Archange Touadera. Bozize alikana madai hayo. Rais mpya atakabidhiwa madaraka ifikapo Machi 30, mwakani.

***RFI***

# Mwandishi wa kwanza kuripoti corona Wuhan afungwa

**Shanghai, CHINA**

MWANDISHI wa habari China, aliyeandika mlipuko wa kwanza wa virusi vya corona katika mji wa Wuhan, amefungwa miaka minne jela.

Zhang Zhan alipatikana na kosa la kuanzisha uvumi na kuzua vurugu na mashtaka mara kwa mara dhidi ya wanaharakati.

Mwandishi mwenye umri wa miaka 37, alizuiwa tangu Mei mwaka huu, huku akigoma kula kwa miezi kadhaa.

Mawakili wake wanasema afya yake imedhoofika vibaya.

Zhang ni mmoja wa wanahabari kadhaa raia wa China waliokuwa mashakani kwa kuripoti kuhusu mwenendo wa virusi vya corona katika eneo la Wuhan.

Hakuna vyombo huru vya habari nchini China na mamlaka inajulikana kwa kuwasaka na kuwachukulia hatua kali wanaharakati wanaoonekana kuhujumu juhudi za serikali kukabiliana na mlipuko huo.

Zhang alifikishwa katika mahakama ya Shanghai akiwa na wakili wake Jumatatu asubuhi.

Kwa mujibu wa mashataka yanayomkabili, alisafiri hadi Wuhan, Februari mwaka huu, kuripoti kuhusu mlipuko wa virusi bila kuzingatia kanuni zilizowekwa.

Ripoti yake aliyoweka mubashara katika mtandao wa kijamii, ilivuma sana Februari, ilimweka mashakani baada ya kuvutia mamlaka za China.

Mtandao wa China wa kutetea haki za binadamu, ulisema ripoti zake zilijumuisha habari za kuwekwa kizuizini kwa waandishi huru wa habari na unyanyasaji wa familia za waathirika ambao walikuwa wakitafuta uwajibikaji.

Zhang alitoweka Wuhan, Mei 14, mwaka huu, kwa mujibu wa CHRD.

Siku moja baadaye, ilifichuliwa kwamba alizuiliwa katika kituo cha polisi cha Shanghai, zaidi ya kilomita 640 kutoka hapo.

Alishtakiwa rasmi Novemba, mwaka huu, nyaraka za mahakama zinasema alitoa taarifa za uongo kupitia ujumbe mfupi, video na kupitia mitandao ikiwamo WeChat, Twitter na YouTube.

Pia anatuhumiwa kwa kukubali kuhojiwa na vya vyombo vya habari vya kigeni kueneza habari za uvumi kuhusu virusi huko Wuhan.

Kifungo cha kati ya miaka minne na mitano kilipendekezwa kutolewa dhidi yake.

Katika hatua ya kulalamikia kukamatwa kwake, Zhang amegoma kula na inasadikiwa kuwa afya yake imekuwa mbaya.

Mmoja wa mawakili wake, alisema katika taarifa kwamba alipoenda kumtembelea mapema Desemba, mwaka huu, alisema atalazimishwa kula kupitia mipira. Pia alisema kuwa anaumwa na kichwa, kuhisi kisunzi na kuumwa na tumbo.

"Kufunga kula kwa saa 24 kwa siku, anahitaji kusaidiwa kwenda masalani, na hapati usingizi," wakili wake Zhang Keke alisema.

"Anapata usumbufu wa kiakili kutokana na dhiki anayopitia kila siku."

Wakili huyo alikuwa amewasilisha mahakamani ombi la kutaka kesi dhidi ya mteja wake kuahirishwa kutokana na hali afya ya Zhang.

Hii sio mara ya kwanza, Zhang kuchukuliwa hatua na mamlaka za China.

Kwa mujibu wa CHRD, aliagizwa kufika polisi mjini Shanghai Septemba 2019 na kuzuiliwa kwa kuunga mkono wanaharakati wa Hong Kong.

***BBC***

## HABARI MICHEZO

# RASHFORD: CAVANI AMEIIMARISHA UNITED

**MANCHESTER, England**

EDINSON Cavani ni "mchezaji wa daraja la juu" ambaye ameipa Manchester United upana wa mashambulizi, amesema Marcus Rashford.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay alijiunga na United kwa uhamisho huru Oktoba baada ya mkataba wake na Paris Saint-Germain kumalizika na ameichezea klabu hiyo jumla ya mechi 13 katika mashindano yote.

Cavani mara nyingi amekuwa akitumika akitokea benchi na mchango wake umekuwa mkubwa zaidi katika siku za hivi karibuni, akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho mbili kwenye mechi sita zilizopita.

Mchango wake wa hivi karibuni ulikuwa Jumamosi iliyopita wakati alipomtengenezea pasi nzuri Bruno Fernandes aliyefunga bao la pili kwa United wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 na Leicester City, na kumfanya Rashford amsifie.

"Ni mchezaji wa daraja la juu, na ana ubora. Nafikiri ametupa nafasi nyingine ya upana zaidi kwenye mashambulizi ambapo ni tofauti na tulivyokuwa mwanzo," alisema akiiambia MUTV.

"Ni vizuri kucheza na yeye na kumuona akifunga na kutoa pasi za mwisho na ni muhimu kwa safu yoyote ya ushambuliaji na tunahitaji kuendelea kuwa kwenye ubora huu."

# MAJERUHI
## YAIANDAMA LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

JOEL Matip alilazimika kutolewa nje kipindi cha pili wakati Liverpool ikitoka sare ya kufungana bao 1-1 na West Brom, na kumuacha kocha Jurgen Klopp kuwa na machaguo machache kwenye safu ya ulinzi.

Mlinzi huyo wa kati, ambaye alianza pamoja na Fabinho, alitolewa nje dakika ya 58 baada ya kuumia nyonga pale kwenye dimba la Anfield, Jumapili na nafasi yake ilichukuliwa na Rhys Williams.

Kikosi cha Klopp sasa kimebakiwa na Williams, Nathanial Phillips na Sepp van den Berg kama ndio walinzi wa kati pekee.

Walinzi nyota wa kati, Virgil van Dijk na Joe Gomez wote wapo nje ya dimba wakiuguza majeraha ya magoti na watakuwa nje kwa muda mrefu.

Kuhusu Matip kulazimika kuondolewa uwanjani kipindi cha pili, Klopp aliwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo: "Joel aliniambia anajisikia maumivu makali kwenye nyonga, kitu ambacho si kizuri.

"Sina uhakika kwa muda gani atakiwa nje ya dimba, lakini alikuwa na maumivu makali na kulazimika kuondolewa uwanjani. Taarifa zaidi mtapata baadaye.

Kwenye mchezo huo, Liverpool walianza kwa kuongoza kwa bao la Sadio Mane la kipindi cha kwanza, lakini Semi Ajayi akasawazisha zikiwa zimesalia dakika nane mpira kumalizika.





# POCHETTINO
## SASA KIMEELEWEKA PSG

**PARIS, Ufaransa**

IMERIPOTIWA kuwa Mauricio Pochettino amesaini mkataba mpya wa kuwa kocha wa Klabu ya Paris Saint-Germain, inayoshiriki Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Mwandishi mkongwe nchini Italia wa masuala ya michezo, Fabrizio Romano, amesema bosi huyo wa zamani wa Klabu ya Tottenham Hotspurs amesaini dili jipya juzi, Jumapili Desemba 27.

Ingawa haijawekwa wazi ni mkataba wa muda gani, lakini mwandishi huyo amethibitisha hilo.

Pochettino anakuwa mrithi wa mikoba ya kocha wa zamani wa PSG, Thomas Tuchel ambaye alifutwa kazi kwa makubaliano na timu hiyo kutokana na mwendo mbovu.

Tuchel alifutwa kazi muda mchache akitoka kuongoza kikosi chake kushinda mabao 4-0 dhidi ya Racing Strasbourg.

Pochettino amekuwa nje kwa muda mrefu bila kuwa na timu baada ya kufutwa kazi ndani ya Klabu ya Spurs mwaka uliopita na amekuwa akihusishwa kujiunga na timu mbalimbai ikiwa ni pamoja na Barcelona, Manchester United na Real Madrid.

## HABARI MICHEZO



# RONALDO

## , GUARDIOLA WABEBA TUZO YA KARNE

**DUBAI, Falme za Kiaarabu**

CRISTINO Ronaldo na Pep Guardiola wametunukiwa tuzo ya Globe Soccer hapa Dubai, na wawili hao wametajwa kama mchezaji bora, na kocha bora wa karne.

Mshambuliaji wa Juventus, Ronaldo alipokea yeye binafsi tuzo hiyo katika sherehe iliyofanyika kwenye Hoteli ya Armani, Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ambaye ameshinda mataji ya ligi katika nchi za Hispania, England na Italia pamoja na Euro 2016 akiwa na Ureno, alibainisha fahari yake kwa kupata tuzo hiyo, ambapo majaji wamemchagua kuwa kwenye kiwango bora zaidi kati ya mwaka 2001 na 2020.

"Ni fahari kushinda mataji," alisema Ronaldo, mshindi mara tano wa Ballon d'Or, katika sherehe hizo.

"Si kazi rahisi kuwa kwenye kiwango cha juu katika mchezo kwa miaka mingi. Najisikia fahari sana, lakini bila timu, makocha wazuri na klabu bora, ni vigumu kufikia mafanikio haya."

Guardiola alitunukiwa tuzo ya kocha bora wa karne kwa kushinda mataji ya ligi kwenye nchi za Hispania, Ujerumani na England, pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili.

Kocha huyo wa Manchester City hakuwapo kwenye sherehe ya tuzo hizo, na alituma ujumbe kupitia video.

Tuzo ya Globe Soccer Awards, ilianzishwa mwaka 2010 kule Dubai kwa ajili ya kutambua mchango wa wanasoka kila mwisho wa mwaka.

## GUNDOGAN AHIMIZA MAN CITY KUIMARIKA




**MANCHESTER, England**

ILKAY Gundogan amedai safu ya ulinzi kwa Manchester City inatakiwa kujiimarisha zaidi na kubaki kuwa na nguvu hata wakati kama hawana wachezaji muhimu wa kushambulia.

City ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Newcastle United Jumamosi kupitia kwa mabao ya Gundogan na Ferran Torres.

Ilikuwa ni mechi yao ya 13 kucheza bila kuruhusu nyavu zao kutikiswa msimu huu kwenye mashindano yote, zaidi ya timu nyingine yoyote kwenye ligi tano bora za Ulaya msimu huu.

"Tumekuwa imara katika safu yetu ya ulinzi," kiungo huyo raia wa Ujerumani, Gundogan aliambia BT Sport.

"Ikiwa tunaweza kuiweka imara safu ya nyuma basi kila wakati tunajipa nafasi kwa sababu tunajua tutafunga mabao.

"Katika kipindi cha kwanza haswa, nilihisi kama tulisogeza mpira vizuri. Hali ya hewa haikuwa nzuri hapa, lakini nadhani tulikuwa na kiwango thabiti."

City ilimkosa Gabriel Jesus, ambaye ana maambukizi ya virusi vya corona, huku Sergio Aguero akitumiwa tena kama mbadala ambapo kocha Pep Guardiola alipunguza mzigo wake wa kazi wakati wa kurudi kutoka kwenye kuuguza majeraha.

Gundogan alisema wachezaji wengine wataendelea kupiga hatua na kuweza kufunga mabao wakati wowote wanapokuwa bila washambuliaji wanaotambuliwa wa timu hiyo.

"Nadhani tunapaswa kushiriki jukumu la kufunga kwenye uwanja kila wakati," aliongeza.



## MODRIC KUONGEZEWA MKATABA REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid inajiandaa kumwongezea mkataba mpya kiungo Mcroatia Luka Modric mwenye umri wa miaka 35, kwa mujibu wa mwandishi wa habari, Fabrizio Romano.

Modric alikuwa anahusishwa na mpango wa kujiunga na Ligi Kuu ya Marekani, MLS, baada ya kumaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu.

Klabu ya La Galaxy ilikuwa tayari kumsajili na kumfanya mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi kwenye MLS.

Modric ameshinda jumla ya mataji 17 akiwa na Real Madrid ikiwamo mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mawili ya LaLiga, moja Copa del Rey [Kombe la Mfalme] na matatu ya Klabu Bingwa Dunia.

Mataji binafsi ni pamoja na tuzo ya kiungo bora wa LaLiga (2016) kwa mara ya pili, kiungo bora wa mashindano ya UEFA mwaka 2017 na 2018.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ATAJA SIKU YA KUONDOKA BARCA

●●●Hakuna kitakachokuwa kigumu kabla ya mwisho wa mwaka, nitasubiri hadi msimu utakapo...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi amebainisha atafanya maamuzi juu ya majaliwa yake pale Barcelona mwishoni mwa msimu huu.

Messi alikaribia kuondoka pale Nou Camp baada ya kuwasilisha maombi ya kuondoka kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini baadaye akaamua kubaki klabuni hapo.

Rais wa zamani wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, alisisitiza kwamba, Messi anatakiwa kuondoka kwa euro milioni 700 ambazo zipo kwenye kipengele cha mkataba wake.

Katika mahojiano na televisheni ya Hispania na La Sexta, aliyoyafanya juzi, sasa ametoa ishara kwa Manchester City, ambao wamekuwa wakihusishwa na mchezaji huyo.

Messi alisema: "Hakuna kitakachokuwa kigumu kabla ya mwisho wa mwaka. Nitasubiri hadi msimu utakapomalizika.

"Ninachojali kwa sasa ni kufikiria kuhusu timu, kumaliza mwaka vizuri na kutohusika kwenye mambo yoyote.

"Sijui nini kitatokea. Kwa sasa naangalia sana nini kilichopo mbele yangu kwa sasa kwa namna yoyote nitakavyoweza.

"Sifikiri namna gani mwaka utamalizika. Halitakuwa jambo la busara kwangu leo hii kuzungumzia nini kinachoendelea kwa sababu sijui."

Wakati akiwa amekataa kuzungumzia wapi anaweza kwenda, Messi alizungumza urafiki wake wa karibu na mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Neymar, na kusema angependa siku moja kucheza naye kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

Man City watakuwa mstari wa mbele kutaka kumsajili Messi kama ataondoka Barcelona, kwa mujibu wa mwandishi wa mtandao wa Goal.com, Jonathan Smith.

"Mara zote nimekuwa na ndoto ya kutaka kucheza kwenye ligi nyingine, hasa Marakeni," alisema.

"Pengine itatokea, kwa sasa siwezi kusema sana. Kwani, kwa sasa naangalia miezi yangu sita iliyobaki kwenye mkataba."

Kuhusu kuungana na Neymar pale Barcelona, Messi alisema: "Litakuwa jambo gumu kusajili wachezaji wengine kwa sababu hakuna fedha.

"Tutaweza kuleta wachezaji kwa ajili ya kuimarisha timu iwe ya ushindani. Lakini Neymar gharama yake itakuwa kubwa sana."

## KWA UFUPI

**OZIL KUPELEKWA JUVENTUS**

ARSENAL imempa ofa kiungo wake, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, kwenda Juventus kwa mkopo wa miezi sita. ***(Tuttosport via the Sun)***

**UNITED NJIAPANDA KWA ALABA**

MANCHESTER United imejiondoa kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Bayern Munich, David Alaba, ambaye anaweza kupatikana akiwa huru kipindi cha majira ya joto. Klabu hiyo ya Old Trafford inaona kwamba gharama itakuwa kubwa zaidi ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, raia wa Austria. ***(The Athletic via Manchester Evening News)***

**ARSENAL KUMCHUKUA LAMPTEY**

ARSENAL ina nafasi nzuri ya kuzipiku Manchester City na Bayern Munich kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa kulia wa Brighton, Tariq Lamptey, mwenye umri wa miaka 20, kama Hector Bellerin mwenye miaka 25, ataamua kwenda katika klabu yake ya utotoni ya Barcelona. ***(Daily Mirror)***

**WIJNALDUM NA MKATABA MPYA**

KIUNGO wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, ataamua kuongeza mkataba wake Liverpool ndani ya siku chache zijazo. ***(The Guardian)***

**VILLARREAL YAITIWA CAPOUE**

KLABU ya Watford imefungua mazungumzo na Villarreal juu ya kumuuza, Etienne Capoue, huku bei yake wakiitaja kuwa ni pauni milioni 4 kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, raia wa Ufaransa. ***(Daily Mail)***

**RICE KUSHAWISHIWA WEST HAM**

KOCHA wa West Ham United, David Moyes ana matumaini kiungo wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 21, anaweza kushawishiwa kuikataa ofa ya Chelsea ili asaini mkataba mpya. ***(Daily Mail)***

**NUNO ATAKA USAJILI WOLVES**

KOCHA, Nuno Espirito Santo amesema Wolves inatakiwa kufanya usajili wakati wa dirisha dogo la Januari ili kuziba pengo la Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 26.***(Sky Sport)***

**BROM KUMBAKIZA JOHNSTONE**

GOLIKIPA wa West Brom, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa na klabu za Leeds United na Brighton, huku klabu yake ikipambana kumbakiza. ***(The Sun).***

**CARRAGHER AWAONYA LIVERPOOL**

NYOTA wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher, amewaonya mabingwa hao kwamba, wanatakiwa kusajili mlinzi mpya wakati wa dirisha la Januari, baada ya kuumia kwa Joel Matip. ***(Sky Sport)***

**JUVE, MILAN KWA EDOUARD**

KLABU za Juventus na AC Milan zimeripotiwa kuingia kwenye mbio moja kuwania saini ya straika wa Celtic, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 22. ***(The Sun)***



HABARI MICHEZO

# MAJIMAJI WALALAMA USINGIZI KIPIGO SIMBA

**Na Adam Fungmwango**

BAADA ya kichapo cha mabao 5-0 dhidi ya Simba kwenye mechi ya Kombe la FA, Kocha Msaidizi wa Majimaji, Gabriel Zacharia, amedai wachezaji wake walikosa muda wa kupumzika kwa sababu walilala usiku wa manane, kwa kuwa waliingia Dar es Salaam saa sita usiku kutokana na kuharibikiwa na gari njiani.

Kocha huyo alisema walitoka Songea tangu Ijumaa, lakini waliwasili Dar es Salaam Jumamosi saa sita usiku huku wachezaji wake wakikosa muda wa kupumzika kutokana na kulala usiku wa manane, na kuchangia zaidi kipigo hicho.

"Kwanza kabisa nawapongeza wachezaji wangu walijituma, lakini wachezaji wangu walikuwa na tatizo la kutokukaba. Na hii yote inatokana na kwamba wachezaji wetu si wazoefu, Majimaji ni timu kubwa, lakini wachezaji ni chipukizi bado hawana uzoefu, lakini pia kingine kilichochangia ni kwamba hawakupata muda wa kupumzika kutokana na tatizo la gari, tulifika Dar es Salaam saa sita usiku," alisema kocha huyo.

Aidha, ameipongeza Simba kwa ushindi huo ambao amedai kuwa walistahili.

Pamoja na Simba kushinda, wanachama na mashabiki wa Simba walionyesha kufurahishwa na mchezaji wa Majimaji Ismail Mussa aliyevaa jezi namba 10, ambaye alionyesha uwezo mkubwa kwenye mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, mchezaji huyo alisema siri ya yeye kuonyesha uwezo wa hali ya juu ni kujituma, kufanya mazoezi kwa bidii na kumsikiliza kocha.

"Tulicheza kwa kuiheshimu Simba, unajua ni timu kubwa. Tumefungwa kutokana na kuwa tumecheza na timu kubwa, lakini kwangu binafsi uwezo nilioonyesha ni kwa sababu ya kujituma na kufanya mazoezi kwa bidii, kumsikiliza kocha, unajua nafanya hivi ili nipate nafasi sehemu nyingine ya kwenda kucheza kwa sababu mpira ni kazi," alisema Ismail.

**UTAMU KOLEA...**




Mtoa pasi ya mwisho, Luis Miquissone akipongezana na mfungaji Meddie Kagere aliyeifungia Simba bao la nne wakati ikishinda mabao 5-0 dhidi ya Majimaji kwenye mechi ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Azam waachana rasmi na Djodi

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umeamua kuachana rasmi na mshambuliaji wao wa kigeni, Richard Djodi, huku nafasi yake ikichukuliwa na kipa kutoka nje ya mipaka ya Tanzania, imefahamika.

Wakati Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', akigoma kutaja mchezaji wanayemtaka ili kupata nafasi ya kusajili mwingine, taarifa za uhakika zilizofikia gazeti hili jana kutoka ndani ya klabu hiyo, Djodi ameondoka ndani ya kikosi cha timu hiyo.

Azam tayari ilikuwa na nyota 10 wa kigeni ambao ni Daniel Amoah, Obrey Chirwa, Prince Dube, Ally Niyonzima, Nicholas Wadada, Bruce Kangwa, Never Tigere, Yakubu Mohammed, Mpiana Moziz na Djodi (ambaye ametemwa), hivyo kwa mujibu wa kanuni za Bodi ya Ligi nchini (TPLB), inaitaka kila klabu kusajili wachezaji wakigeni 10 pekee, jambo ambalo klabu hiyo ilipaswa kupunguza waliopo ili kupata nafasi mpya ya kusajili.

Popat alisema baada ya Kocha Mkuu, George Lwandamini, kuona upungufu uliopo katika kikosi chake, alihitaji kusajiliwa mshambuliaji, hivyo kumsajili Mpiana huku suala la kipa likiwa katika mchakato.

"Kulingana na idadi ya wachezaji 10 wa kigeni walikuwapo ndani ya timu, lazima mmoja atoke ili mwingine aingie, kwa sasa ni mapema kutaja ni nani ila mambo yakiwa sawa tutaweka wazi ni mchezaji gani," alisema Popat. Lakini chanzo chetu cha uhakika ndani ya klabu hiyo, kimeweza kuwa tayari, Djodi ameondoka nchini (tangu Ijumaa) baada ya kuvunjwa kwa mkataba wake na kupewa stahiki zake.

"Djodi ametemwa rasmi na nafasi yake kuchukuliwa na kipa wa kigeni ambaye kwa sasa bado hajajulikana baada ya Kocha Mkuu Lwandamina, kukabidhi jina la kipa," kilieleza chanzo chetu.

## Mngazija atoa siri Chuoni kushinda

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kushinda mechi yake ya pili mfululizo kwenye kinyang'anyiro cha Ligi Kuu Zanzibar, Kocha Mkuu wa timu ya Chuoni, Ali Bakari Mngazija, amesema matokeo hayo yanatokana na kupata muunganiko mzuri kikosini.

Juzi Chuoni iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Maafande wa Zimamoto katika mfulululizo wa ligi hiyo kwenye mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Amaan.

Mabao ya Chuoni yalifungwa na Halid Abibu dakika ya 24 na Mundhir Abdallah dakika ya 84, huku lile la kufutia machozi kwa Zimamoto likifungwa na Haruna Abdalla dakika ya 23.

Chuoni ambayo sasa imefikisha alama saba ikiwa nafasi ya 11 kwenye msimamo wa ligi hiyo, ilikuwa katika hali mbaya baada ya kupoteza mechi nne za mwanzo na kutoka sare moja, lakini juzi ilishinda mechi yake ya pili mfululizo jambo ambalo kocha huyo amelitolea ufafanuzi.

"Wachezaji wanacheza vizuri na wanajituma, kwa sasa wachezaji wapata muunganiko na kuyafanyia kazi maelekezo ninayopata kabla na hata katika mchezo ili kuhakikisha timu haitoki na matokeo mbaya.

"Malengo yangu ni kuhakikisha natoka katika mstari mwekundu wa kushuka daraja na kufikia katika nafasi ambazo tutajiweka salama," alisema Mngazija.

## Sababu Mwenyekiti Mlandege kujiuzulu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu wa 2019-2020, Klabu ya Mlandege, Mbaraka Himid, amejiuzulu nafasi yake hiyo.

Kwa mujibu wa barua aliyoandika mwenyewe kwa uongozi wa Mlandege, imeeleza kujiuzulu kwake kumetokana na kubanwa na majukumu ya kikazi hali ambayo mara nyingine imekuwa ikimsababishia kushindwa kutekeleza majukumu ya klabu.

Akithibitisha kujiuzulu kwa mwenyekiti wa timu hiyo, Katibu Mkuu wa Mlandege, Salum Mohmed, alikiri kupokea barua hiyo na kueleza bado uongozi haujakutana kuijadili.

"Uongozi wa Mlandege utatoa taarifa baadaye baada ya kukutana na kuona namna ya kujaza nafasi hiyo," alisema katibu huyo.


Aidha, aliwataka mashabiki wa Mlandege kutulia na kusubiri uongozi wao hadi utakapotoa taarifa nyingine baada ya kupokea barua hiyo ya kujiuzulu kwa mwenyekiti wao.

Timu ya Mlandege ipo nafasi ya nane katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama nane baada ya kushinda michezo miwili na sare mbili na kupoteza mechi mbili.

# Michezo

Jumanne Desemba 29, 2020

Nipashe

MESSI ATAJA SIKU YA KUONDOKA BARCA HABARI UK 22

MBINU MBADALA...



Mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane, akipata upinzani kutoka kwa beki wa West Brom, ambaye ameamua kumkumbatia ili kumpunguza kasi asisababishe madhara langoni mwao kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## KAZE APANIA REKODI YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Tanzania Prisons kujinasibu kwamba itatibua rekodi ya Yanga ya kutopoteza mechi hadi sasa, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema matokeo ya kumaliza mzunguko wa kwanza kwa kuwa kileleni, yanawapa ari ya kuendeleza ushindi mzunguko wa pili.

Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 43, imemaliza mechi 17 za mzunguko wa kwanza bila kupoteza, ikishinda 13 na kutoka sare michezo minne.

Hata hivyo, juzi Katibu Mkuu wa Prisons, Ajibu Kifukwe, alisema anakumbuka msimu uliopita Prisons ilikuwa ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mechi hata moja kwenye Ligi Kuu, lakini Yanga ndiyo ilitibua rekodi hiyo, kwa hiyo na wao wamejipanga kulipiza kisasi kwa kuwaharibia rekodi yao ya kutopoteza pia.

Lakini Kaze amesema, wachezaji wake watazidi kupambana ili kuwa bora kwenye mechi zao zijazo za mzunguko wa pili.

"Tuna kila sababu ya kushukuru kumaliza mzunguko wa kwanza tukiwa tunaongoza msimamo wa ligi, hii ni kutokana na wachezaji kujitoa na kujitambua kuhakikisha tunapata pointi tatu katika kila mchezo ambazo zimetufikisha hapa.

"Natumaini tutaanza tena vizuri mzunguko wa pili ili tuweze kufanikiwa kufanya vizuri na mwisho wa siku tutwae ubingwa wa ligi," alisema Kaze.

Timu hizo zitashuka Dimba la Nelson Mandela mjini Sumbawanga keshokutwa, Alhamisi zikiwa na kumbukumbu ya kutoka sara ya bao 1-1 katika mchezo wa raundi ya kwanza uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# SVEN ACHEFUKA SIMBA

## ●●●Asema lawama zote abebeshwe yeye, wachezaji wake wasiguswe kwa sababu wanaipigania timu, huku...

**Na Saada Akida**

HUKU akitambua bado ana mlima mrefu wa kupanda kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na kutetea mataji yake mawili, Ligi Kuu Bara na Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amechefuka kutokana na wachezaji wake kukosolewa mara kwa mara, ameeleza.

Simba kesho, Jumatano itaikaribisha Ihefu FC Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mchezo wa raundi ya pili wa Ligi Kuu Bara, wakati huu ikiwa nafasi ya pili kwenye msimamo na alama zake 32, nyuma ya Yanga yenye pointi 43, lakini ikiwa mbele mechi tatu.

Lakini Sven amesema kwa sasa lawama zote kuhusu uwezo wa wachezaji wake ndani ya uwanja anapaswa kupewa yeye na hataki kuona mashabiki ama vyombo vya habari wakiwakosoa.

Akizungumza baada ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Majimaji FC kwenye mechi ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, kwa hasira Sven alisema amekuwa akisikia maneno kuhusu uwezo wa wachezaji wake pamoja na matokeo ambayo wanayapata ndani ya uwanja akishinda hata anapofungwa.

"Tulikuwa Nigeria hivi karibuni na tulishinda bao 1-0 ila watu walikuwa wanasema kuhusu wachezaji wangu pamoja na matokeo ambayo tunayapata.

"Sitaki kuona yeyote kutoka vyombo vya habari ama mashabiki kukosoa wachezaji wangu kwani wanajitoa kwa kila kitu kupigania jezi hii, mkitaka nikosoeni mimi.

"Haijalishi tunafungwa ama tunashinda bado hawastahili lawama iwe ni kwa mashabiki wale waliopo ndani ya timu pamoja na vyombo vya habari, sitaki kusikia kuhusu wachezaji wangu wakilaumiwa nataka kulaumiwa mimi.

"Hivi karibuni kuna mchezaji wangu hakusafiri na timu na bado ni mgonjwa [Bernard Morrison], na amekuwa akiipambania sana timu, lakini bado wapo wanaomkosoa," alisema Sven.

Kuhusu mechi ya kesho dhidi ya Ihefu FC, Sven alisema anachohitaji ni pointi tatu muhimu na kwamba kila mechi ni muhimu na hufanya maandalizi kulingana na mchezo husika.

Alisema kabla ya kurudiana na FC Platium kwenye mechi ya raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wana mechi ngumu ya ligi ambayo wanahitaji matokeo mazuri ili kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kutetea ubingwa.

"Tumeanza vizuri mechi ya leo (juzi) ya FA dhidi ya Majimaji, nawapongeza wachezaji wangu kwa ushindi wa mabao 5-0, mapambano yanaendelea na sasa tunajipanga kwa mechi yetu dhidi ya Ihefu FC," alisema Sven.

Alisema wanahitaji kupata pointi tatu muhimu, na ana imani mechi hiyo ya ligi itakuwa kipimo tosha kuelekea mchezo wa marudiano dhidi ya Platinum kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tuna nafasi ya kufanya vizuri katika mechi dhidi ya FC Platinum, nina imani baada ya mechi dhidi ya FA, tutazidi kuimarika na kufanya vizuri zaidi mechi yetu hiyo ya kimataifa," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Katika mechi hiyo ya FA, mabao ya Simba yalifungwa na beki Gadiel Michael dakika ya tatu, mshambuliaji Mkongo Chris Mugalu (dk. 6), beki Ibrahim Ame (dk. 60), straika Mnyarwanda Meddie Kagere (dk. 78) na kiungo kutoka Msumbiji, Luis Miquissone dakika ya 90.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002